# Nipashe

Alhamisi Novemba 12, 2020 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580397

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710 LIKE & FOLLOW US


**MAGUFULI** kutoa picha miaka mitano ijayo kesho akizindua Bunge la 12

UKURASA 2



**ADAIWA** kumuua mchumba wa zamani kwa tuhuma kumroga kwenye ndoa

UKURASA 4




UKURASA 11

# NEC yaikana orodha wabunge Viti Maalum

**• Yakiri** haijapokea majina kutoka CHADEMA, Lissu atoa msimamo... *Endelea ukurasa 2, 4*



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi (kulia), akisalimiana na Spika wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar, Zuberi Ali Maulid, kabla ya kulihutubia baraza hilo, Chukwani Zanzibar jana. **PICHA: IKULU ZANZIBAR**

## KUMRADHI

KATIKA toleo letu la Jumatatu, Novemba 9, 2020 tulichapisha taarifa yenye kichwa cha habari 'Saruji haishikiki' na kichwa cha habari kidogo: 'Yaadimika kila mahali nchini, mfuko wafikia 35,000/- wananchi waiangukia serikali'.

Hata hivyo, kwa mujibu wa mamlaka tulizowasiliana nazo kuhusu bei ya saruji katika eneo la Loliondo na Ngorongoro, mkoani Arusha, bei hiyo haizidi Sh. 25,000 kwa mfuko mmoja.

Kwa mujibu wa mamlaka hizo, mfuko mmoja Arusha ulinunuliwa kwa Sh. 17,000 na ukisafirishwa hadi Ngorongoro na Loliondo unauzwa kwa Sh. 23,000, hata ukipanda hauzidi Sh. 25,000.

Tunaomba radhi kwa wasomaji wetu na mamlaka husika kwa taarifa hiyo ambayo ilikuwa na upotoshaji wa bei ya Sh. 35,000 ambayo iliuzwa kilanguzi na kutofuatilia kwa umakini kwa mamlaka husika.

**Mhariri**

# Corona yakwamisha mradi wa Jangwani

UKURASA 2

# Dk. Mwinyi ataja sifa mawaziri atakaoteua

UKURASA 3




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play App Store

SALAMU ZA PONGEZI



Gazeti Nipashe linampongeza Rais Dkt John Magufuli na Makamu wa Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuchaguliwa tena kwa kipindi kingine cha Miaka 5. 2020 - 2025

Kwa salamu za pongezi
Wasiliana nasi kwa Simu: 0686 101335
Barua pepe: advertise@guardian.co.tz



SALAMU ZA PONGEZI

# NEC yaikana orodha wabunge CHADEMA

**Na Allan Isack,** ARUSHA

TUME ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), imesema haijapokea orodha ya majina ya wabunge wa viti maalumu kutoka Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA).

Akizungumza na Nipashe jana kwa njia ya simu, Mkurugenzi wa Uchaguzi wa NEC, Dk. Wilson Mahera, alisema tume bado haijapokea orodha hiyo kama ambavyo imekuwa ikisambazwa kwenye mitandao ya kijamii.

"Kuna orodha ya majina inayosambaa kwenye mitandao ikionyesha majina ya wabunge wa Viti Maalumu wa CHADEMA. Orodha hiyo si ya kweli kwani hadi sasa hatujapokea orodha ya majina ya walioteuliwa kwenye nafasi ya ubunge wa viti maalumu kutoka chama hicho," alisema.

Mkurugenzi huyo alisema amesikitishwa na taarifa ya Katibu Mkuu wa CHADEMA, John Mnyika, iliyodai kuwa orodha ya majina hayo ni ya tume.

"Tume tumesikitishwa sana kusikia Katibu wa CHADEMA, John Mnyika, akidai kuwa orodha ya majina ya wabunge wa viti maalumu ni ya tume. Imetusikitisha sana kwa kuwa siyo kweli," aliongeza.

Dk. Mahera alisema aliwasiliana na Mnyika kwa kumpigia simu na kumwandikia barua ya kuulizia orodha ya majina hayo na kumwambia asubiri mpaka atakapoyaleta yeye mwenyewe baada ya utaratibu wa chama kukamilika.

"Mnyika mwenyewe anafahamu kuwa bado hatujapokea majina na alisema atayaleta majina hayo yeye mwenyewe endapo watakamilisha utaratibu wao, hivyo mpaka sasa hivi, NEC hatujapokea majina kutoka CHADEMA ambayo yamesainiwa na Katibu Mkuu wa chama hicho," alisema Mahera.

"Bado tunasubiri majina hayo ambayo yametiwa saini na kupigwa muhuri wa Katibu Mkuu wa chama kwa kuwa utaratibu ndio unaelekeza hivyo," alisisitiza.

Kutokana na kuvuja kwa orodha hiyo, kuna taarifa kwamba Mnyika alimwandikia barua Dk. Mahera, kutaka kupewa ufafanuzi kama tume imeshatangaza na kuwasilisha bungeni majina 19 ya wabunge wa viti maalumu wa chama hicho.

Aidha, tangu kutoka kwa majina hayo kwenye mitandao, kumekuwa na taharuki juu ya chanzo halisi cha majini hayo, huku wapinzani, wakiwamo CHADEMA, wakiirushia lawama NEC kuwa ndiyo imehusika.

## JPM kulifungua Bunge kesho

**Na Romana Mallya,** DODOMA

RAIS John Magufuli anatarajiwa kulifungua na kulihutubia Bunge la 12 kesho katika mkutano wake wa kwanza ulioanza juzi.

Spika wa Bunge, Job Ndugai, alitangaza hayo bungeni jana jijini hapa baada ya kuwa amewaapisha wabunge 361.

Wakati hayo yakiendelea, nafasi ya Waziri Mkuu na Naibu Spika hadi jana zilikuwa bado hazijajazwa.

Spika Ndugai alisema Rais Magufuli atahutubia Bunge hilo ili kuweka dira ya serikali yake kwa miaka mitano ya utekelezaji wa ilani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) kadri anavyoona inafaa.

"Ninawaomba wabunge wote muwe ndani ya ukumbi kuanzia saa tatu asubuhi, maelekezo mengine mtayapata siku hiyo, tutaanza na gwaride hapo nje, tutakuwa na wageni wengi hivyo muwahi," aliagiza.

Spika Ndugai pia aliwataka wabunge wote ambao wako nje ya Dodoma, warejee katika jiji hilo jipya kwa ajili ya kusikiliza hotuba hiyo ya Rais.

Rais Magufuli atahutubia Bunge hilo likiwa na wabunge wengi zaidi wa chama kilichoko madarakani kulinganishwa na Bunge la 11 ambalo lilikuwa na wabunge zaidi ya 100 vyama vya upinzani.

Safari hii Bunge hilo lina wabunge wa CCM walioshinda majimboni 256 na 94 wa viti maalum. Katika Uchaguzi Mkuu wa Oktoba 28 mwaka huu, CCM ilishindwa majimbo mawili Tanzania Bara na sita visiwani Zanzibar.

Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) ni chama pekee cha upinzani kilichokidhi masharti ya kuwa na wabunge wa viti maalum bungeni, safari hii kikiambulia nafasi 19 tu.

Hata hivyo, chama hicho bado hakijawasilisha kwa Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) majina ya wabunge hao wanaohitajika kwenda bungeni kula kiapo, kikiweka msimamo wa kutoyakubali matokeo ya Uchaguzi Mkuu wa Oktoba 28, mwaka huu, ambao kimeambulia jimbo moja.



Sehemu ya Barabara ya Morogoro, ikiwa imejaa tope na mchanga katika eneo la Jangwani, jijini Dar es Salaam jana, kutokana na mvua inayonyesha na kusababisha usumbufu kwa watumiaji wa barabara hiyo. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## KUMRADHI

**KATIKA toleo letu la Jumatatu, Novemba 9, 2020 tulichapisha taarifa yenye kichwa cha habari 'Saruji haishikiki' na kichwa cha habari kidogo: 'Yaadimika kila mahali nchini, mfuko wafikia 35,000/- wananchi waiangukia serikali'.**

**Hata hivyo, kwa mujibu wa mamlaka tulizowasiliana nazo kuhusu bei ya saruji katika eneo la Loliondo na Ngorongoro, mkoani Arusha, bei hiyo haizidi Sh. 25,000 kwa mfuko mmoja.**

**Kwa mujibu wa mamlaka hizo, mfuko mmoja Arusha ulinunuliwa kwa Sh. 17,000 na ukisafirishwa hadi Ngorongoro na Loliondo unauzwa kwa Sh. 23,000, hata ukipanda hauzidi Sh. 25,000.**

**Tunaomba radhi kwa wasomaji wetu na mamlaka husika kwa taarifa hiyo ambayo ilikuwa na upotoshaji wa bei ya Sh. 35,000 ambayo iliuzwa kilanguzi na kutofuatilia kwa umakini kwa mamlaka husika.**

***Mhariri***

# Corona yakwamisha mradi wa Jangwani

**Na Christina Mwakangale**

MRADI wa ujenzi eneo la Jangwani ili kuondoa adha inayowakabili wakazi wa Jiji la Dar es Salaam, kufungiwa Barabara ya Morogoro kila zinaponyesha mvua, umekwamishwa na mlipuko wa virusi vya corona.

Mpango huo ulitarajiwa kuanza mwaka huu ukitekelezwa na Jiji, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) kwa kushirikiana na Benki ya Dunia (WB).

Mkurugenzi wa Jiji Dar es Salaam, Sipora Liana, aliyasema hayo jana jijini, akibainisha kwamba: "Ilitakiwa kuanza kufanyika mapema mwaka huu, lakini kila kitu kilisitishwa kutokana na hili.

"Pale Jangwani tatizo ni maji kujaa na kushindwa kutoka. Kwa hiyo, baada ya hii Covid-19, ninataka turudi TAMISEMI ili kujua inatakiwa kuanza lini, mratibu alihamishwa, inabidi nifuatilie tena, sijajua utaanza lini," alisema Liana.

Alisema eneo la Jangwani litakuwa la kuvutia kwa ajili ya mapumziko, michezo na makazi ya watu.

"Ninajaribu kuomba ofisa aliyekuwa anaratibu niongee na Katibu Wizara ya Ardhi ili arudishwe tuendelee na mkakati. Kama ilivyo katika majiji mengine duniani, mito inayokatiza katikati ya miji haileti adha kwa wakazi," alisema.

Alibainisha kwamba eneo hilo ambako Mto Msimbazi unakatiza, utachimbwa mtaro kuelekea baharini, kuruhusu maji kwa urahisi.

"Awali tulishirikisha wananchi katika mpango huu kwa ambao walirudi Jangwani, waondolewe, wanaotakiwa kulipwa walipwe, halafu mto uchimbwe kuelekea baharini," alibainisha.

Dereva wa daladala anayetumia Barabara ya Morogoro, Andrea Mwasha, alisema eneo la Jangwani linapojaa maji na barabara kufungwa, kazi inakuwa ngumu kutokana na kushindwa kukamilisha hesabu ya siku.

"Kawaida gari za masafa marefu labda Masaki-Kigogo, hesabu zetu ni safari tano hadi sita siku nzima. Sasa, ikifungwa barabara, malengo hayatimii sababu foleni inakuwa kubwa, utakuta umefanya 'ruti' tatu," alilalamika.

Mkazi wa Mwenge, Yasinta Mushi, ambaye ni mfanyabiashara wa Kariakoo, alisema serikali itoe kipaumbele cha ujenzi wa daraja la juu eneo la Jangwani kama ilivyofanyika Ubungo na TAZARA.

"Hii Barabara ya Morogoro inategemewa na wakazi wa jiji kwa asilimia kubwa, ila kikwazo Jangwani mvua ikinyesha. Inakubidi utumie gharama nyingine ya ziada kufika uendako na kuchelewa pia," alisema Yasinta.

Juzi, Jeshi la Polisi Kanda Maalum Dar es Salaam, lilifunga baadhi ya barabara hususan zinakokatiza Mto Msimbazi ikiwamo ya Barabara ya Morogoro baada ya kufurika maji eneo la Jangwani.

Kamanda wa Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Lazaro Mambosasa, aliiambia Nipashe kwamba pamoja na mvua hiyo kutoleta madhara ya moja kwa moja kwa binadamu, jeshi hilo lilichukua tahadhari kwa kufunga barabara ambazo mito hufurika.

"Tumefunga njia, Jangwani, Kigogo kuna wakati tulifunga wakati maji yakikupwa kwa ajili ya kudhibiti watu wasiende, wabaki salama," alisema Mambosasa.

# Mwinyi atoa sifa mawaziri wapya

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amefungua rasmi Baraza la 10 la Wawakilishi Zanzibar, akisisitiza uteuzi wake wa viongozi, wakiwamo watakaounda Baraza la Mawaziri, utazingatia uwezo wa mtu kitaaluma, uwajibikaji na uadilifu.

Katika hotuba yake ya ufunguzi wa baraza hilo jana, Dk. Mwinyi alisema serikali yake haitakuwa na kigugumizi katika kumwajibisha mtendaji yeyote ambaye atashindwa kuwajibika na kuleta ufanisi katika sehemu za kazi.

Alisema wateule wake atakaowachagua, anataka wawe na uwezo na ubunifu wa kitaaluma kwa ajili ya kuleta ufanisi na hatawavumilia watendaji watakaobainika kujishughulisha na vitendo vya rushwa na ufisadi.

Dk. Hussein alisema yuko tayari kuwatumikia wananchi wa Zanzibar pamoja na kushirikiana na makundi yote vikiwamo vyama vya siasa na kutekeleza maridhiano ya kisiasa ya serikali ya umoja wa kitaifa ambayo yapo kwa mujibu wa katiba, ili kujenga taifa lenye mshikamano na uchumi imara. "Huu ni wakati wa kujenga mshikamano na kuachana na chuki za kisiasa ambazo zimekuwa zikirudisha nyuma maendeleo ya wananchi," alisema.

Aliwataka wajumbe wa baraza hilo kuwa tayari kuwatumikia wapigakura wao katika majimbo ya uchaguzi na serikali itatoa ushirikiano wa karibu na kuzipatia ufumbuzi kero mbalimbali zinazowakabili katika majimbo.

"Ndugu wananchi, ninapenda kuwajulisha kwamba serikali yenu sasa ipo tayari kufanya kazi na kushirikiana na ninyi katika kuleta maendeleo na kukabiliana na kero mbalimbali.

"Ninawaomba wajumbe wa Baraza la Wawakilishi mliochaguliwa na wapigakura, fanyeni kazi zenu kwa mujibu wa sheria... nipo tayari kutoa ushirikiano kwenu," alisema.

Alisema serikali yake imejipanga vizuri kuhakikisha sekta zote ikiwamo binafsi zinashirikishwa kikamilifu katika ujenzi wa taifa ikiwamo sekta ya utalii na kufikia kupokea watalii 850,000 kwa mwaka.

Alisema amefurahishwa kuona idadi kubwa ya watalii wanaingia nchini licha ya kuwapo kwa ugonjwa wa corona katika baadhi ya nchi duniani.

Dk. Mwinyi pia alisema anakusudia kukitangaza Kisiwa cha Pemba na kukifanya kuwa eneo maalumu la uwekezaji kiuchumi ikiwamo kujenga bandari za kisasa katika miji ya Mkoani, Shumba na Wete.

Alisema anakusudia kujenga viwanda mbalimbali kwa kushirikiana na wawekezaji na ujenzi wa bandari zitakazofanya kazi kwa kushirikiana na nchi jirani kwa lengo la kukuza uchumi.

Alisema serikali yake itahakikisha inapambana na ufisadi wa mali za umma pamoja na kuwachukulia hatua watendaji ambao hawako tayari kufanya kazi kwa maslahi ya taifa, huku wakijifikiria wao wenyewe kujinufaisha kwa malengo binafsi.

"Nitahakikisha watendaji ninaowateua ni wale wenye sifa na vigezo vya elimu na uwajibikaji, ndiyo nitakaowapa nafasi ya kufanya kazi na kushika nafasi za uongozi katika taasisi mbalimbali," alisema.

Dk. Mwinyi alieleza masikitiko yake ya kutoridhishwa na utendaji wa kazi katika Bandari ya Malindi na Uwanja wa Ndege wa Abeid Amani Karume ambako kumekuwapo na uzembe na upotevu wa mali katika maeneo ya ukusanyaji wa fedha zinazoingia kupitia vyanzo hivyo vya mapato.

"Baada ya kuapishwa tu nilifanya ziara katika Bandari ya Malindi na kujionea msongamano mkubwa wa makontena, lakini sijaridhishwa na utendaji wa kazi katika Uwanja wa Ndege wa Abeid Amani Karume. Ukusanyaji wa mapato hauridhishi hata kidogo, hivyo nitafanya ziara za mara kwa mara katika maeneo hayo," alisema.

Dk. Mwinyi alisema serikali itaendelea kuboresha huduma muhimu na kuzifanya kuwa bure kama zilivyoasisiwa na Hayati Abeid Amani Karume ikiwamo matibabu bure na elimu bila ya malipo.

Alisema atahakikisha wajasiriamali wanasajiliwa na kutambuliwa pamoja na kupewa vitambulisho vitakavyowawezesha kulipa kodi mara moja kwa mwaka.

Uzinduzi wa baraza hilo la wawakilishi ulihudhuriwa na viongozi mbalimbali wa ngazi za kitaifa wakiwamo marais wastaafu wa Jamhuri ya Muungano pamoja na Zanzibar akiwamo Ali Hassan Mwinyi, Dk. Ali Mohamed Shein, Amani Abeid karume, Makamu wa Pili mstaafu, Balozi Seif Ali Iddi, Jaji Mkuu wa Zanzibar, Omar Othman Makungu na mabalozi.



Marais wastaafu wakifuatilia hotuba ya Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi (hayupo pichani), wakati wa ufunguzi wa Baraza 10 la Wawakilishi Zanzibar jana. Kutoka (kushoto) ni Rais mstaafu wa Tanzania, Ali Hassan Mwinyi, Marais wastaafu wa Zanzibar, Dk. Amani Abeid Karume na Dk. Ali Mohammed Shein na Makamu wa Pili wa Rais mstaafu, Balozi Seif Ali Iddi. **PICHA: IKULU ZANZIBAR**

# Mwakilishi afariki dunia kabla ya kuapa

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

ALIYEKUWA Waziri wa Katiba na Sheria Zanzibar ambaye ni Mwakilishi mteule wa Jimbo la Pandani kwa tiketi ya ACT-Wazalendo, Abubakar Khamis Bakari, amefariki dunia usiku wa kuamkia jana nyumbani kwake Mbweni nje kidogo ya mji wa Unguja.

Spika wa Baraza la Wawakilishi, Zubeir Ali Maulid, alitoa taarifa hiyo mbele ya wajumbe wa Baraza la Wawakilishi muda mfupi wakisubiri hotuba ya Rais wa Zanzibar, Dk.Hussein Ali Mwinyi, kulizindua baraza hilo.

Maulid alisema Ofisi ya Spika imepokea taarifa za kifo cha mwakilishi mteule Abubakar kwa huzuni kubwa kwa sababu kwa nyakati tofauti alikuwa mtumishi wa taasisi hiyo pamoja kuwa mwakilishi na waziri.

Alieleza Abubakar alichaguliwa na wananchi wa Jimbo la Pandani kuwa mwakilishi wao katika uchaguzi mkuu wa Oktoba 28, lakini kwa bahati mbaya hakuwahi kuapishwa. "Ofisi yetu imepokea taarifa za msiba wa mwakilishi mteule Abubakar Khamis Bakary ambaye alichaguliwa na wananchi wa Jimbo la Pandani ingawa hakula kiapo," alisema. Maulid alitoa pole kwa wananchi wa jimbo hilo, kwa kuondokewa na mwakilishi wao ambaye walimchagua kwa kumpigia kura nyingi.

Bakary aliibuka na ushindi katika Jimbo la Pandani lililopo Wete Pemba katika kinyang'anyiro cha nafasi ya uwakilishi na kukifanya Chama cha ACT-Wazalendo kupata majimbo manne Pemba.

Ndiye Katibu wa kwanza Baraza la Wawakilishi 1980, huku akihusika katika mchakato wa kuundwa kwa katiba ya kwanza ya Zanzibar ya mwaka 1984 wakati wa uongozi wa Aboud Jumbe Mwinyi.

Mwaka 1984 - 1988 alikuwa Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar, na mwaka 1989-1990 alikuwa Naibu Jaji Mkuu wa Zanzibar.

Kuanzia mwaka 2005-2010 alikuwa mwakilishi Jimbo la Mgogoni Pemba na katika kipindi cha Serikali ya Umoja wa kitaifa chini ya uongozi wa Dk. Ali Mohamed Shein mwaka 2010 Abubakar aliteuliwa kuwa Waziri wa Katiba na Sheria. Marehemu amebobea zaidi katika masuala ya uandishi wa katiba na miswada mbalimbali katika vyombo vya kutunga sheria.

Akilihutubia Bunge wakati wa uzinduzi wa baraza hilo, jana, Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, alisema amepokea kwa huzuni kubwa kifo cha kiongozi huyo ambaye alikuwa Mjumbe wa Baraza Kuu la Chama cha ACT-Wazalendo.

## RC Dar awatangazia kiama walanguzi saruji

**Na Mwandishi Wetu**

MKUU wa Mkoa wa Dar es Salaam, Aboubakar Kunenge, ameagiza maduka yote yanayouza saruji kwenye mkoa huo kuhakikisha yanauza kwa bei elekezi.

Ameagiza kuwa bei hiyo isizidi Sh. 15,000 na kumuelekeza Kamanda wa Polisi Kanda Maalumu ya Dar es Salaam, Lazaro Mambosasa, kuanza msako wa kuwakamata wote watakaokiuka agizo hilo.

Kunenge alitoa agizo hilo wakati wa ziara kwenye viwanda vinavyozalisha saruji na maduka yanayouza saruji mkoani, ambapo alishangazwa kuona uzalishaji wa saruji kwenye viwanda ukiendelea kama kawaida na kuuza kwa bei ya Sh. 12,500, lakini wauzaji wanauza kwa bei ya Sh. 17,000.

Mkuu wa mkoa alipowauliza kwa nini wanauza kwa bei hiyo, walieleza kwamba wanauziwa kwa bei ya Sh. 14,500 kutoka kwa kawakala, kitendo alichokiita kuwa ni hujuma.

Kutokana na hali hiyo, Kunenge alitoa maelekezo kwa ofisa biashara wa mkoa huo kupitia upya utaratibu wa uzalishaji na uuzaji wa saruji kuanzia ngazi ya kiwandani hadi kwa mtumiaji wa mwisho ili kudhibiti upandaji holela wa bei.

Aidha, Kunenge alisema ameandaa kikosi kazi kitakachopita kwenye maduka jijini humo na kuwakamata wote watakaouza saruji kwa bei tofauti na iliyoelekezwa.

"Katika Mkoa huu chini ya Rais Dk. John Magufuli hatuwezi kukubali upuuzi wa aina hii, hatukubali hujuma hii na hatukubali uroho na ulafi wa watu wachache wanaoumiza wananchi kwa maslahi yao binafsi... kuanzia wakati huu saruji kwenye mkoa huu isiuzwe zaidi ya shilingi 15,000," alisema Kunenge.

Kwa upande wake Mambosasa alisema jeshi hilo limejipanga ipasavyo kuhakikisha wanafuatilia maeneo yote ya jiji hilo, na kuwawajibisha watakaokiuka maelekezo hayo.

# Mbaroni madai kumuua mpenzi wa zamani akimtuhumu kumroga

**Na Halima Ikunji,** TABORA

KURWA Langi (50) mkazi wa Urambo mkoani Tabora, Kurwa Langi (50), anashikiliwa na jeshi la polisi kwa tuhuma za kumuua Kumbi Shija, mkazi wa Kata ya Kiloleni, kwa madai kuwa amemroga ashindwe kufanya tendo la ndoa.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Tabora, Barnabas Mwakalukwa, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo lililotokea Novemba 8, mwaka huu, usiku.

Mwakalukwa alisema mauaji hayo yametokea baada ya baadhi ya waganga wa kienyeji kupiga ramli chonganishi kwa madai kuwa Shija amehusika kumroga mtuhumiwa hivyo kushindwa kufanya tendfo la ndoa.

Kutokana na mauaji hayo, alisema waganga waliohusika watakamatwa na kuhojiwa kisha sheria itachukua mkondo wake.

Alisema Langi alipohojiwa aliwaambia polisi kuwa alichukua uamuzi huo baada ya kwenda kwa mganga wa kienyeji na kuambiwa kwamba Shija ambaye aliwahi kumchumbia ndiye anayemroga.

Mtuhumiwa huyo, kwa mujibu wa Mwakalukwa, alisema aliwahi kumposa binti huyo na baadaye kughaili kumuoa na kwenda kuoa mwanamke mwingine.

Alisema baadaye, akiwa kwenye ndoa yake, alikuwa akishindwa kutekeleza jukumu la ndoa kwa mke wake na alipoona tatizo hilo, aliamua kwenda kwa waganga wa kienyeji watano ambao wote walimwambia amerogwa na mwanamke aliyemchumbia na kumwacha.

"Kutokana na kuambiwa huko waganga hao, Langi aliamua kwenda kutekeleza mauaji hayo," alisema Mwakalukwa.

Ofisa Mtendaji wa Kata ya Kiloleni, Amos Nicholas, alisema Shija alifia hospitalini katika karakati za kuokoa maisha yake

Alisema baada ya kushambuliwa na mchumba wake huyo wa zamani, walimpeleka mwanamke huyo hospitalini lakini alifia mikononi mwa madaktari kwa sababu alikatwa sehemu mbaya.

Ofisa Tarafa wa Tarafa wa Usoke, Nelson Majula, alitoa pole huku akisema ama ilivyokuwa sheria ya kata ya Tarafa ya Usoke huku mwanamume aliyemkaribisha mtuhumiwa huyo anayejulikana kama Issa Mohamed mkazi wa Kata ya kiloleni naye amejikuta hatiani baada ya kumkaribisha mgeni pasipo kufuata taratibu za kijiji.



Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Aboubakar Kunenge (mwenye kofia), akikagua moja ya maduka yanayouza saruji, jijini humo jana, kutokana na bidhaa hiyo kupanda bei ghafla. Wa (pili kushoto) ni Kamanda wa Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Lazaro Mambosasa. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Lissu aonya CHADEMA uteuzi wa viti maalum

**Na Mwandishi Wetu**

MAKAMU Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Tundu Lissu, amesema wanachama watakaokubali viti maalum bila utaratibu wa chama, watakuwa wamekubali kilicho haramu.

Akizungumza jijini Dar es Salaam muda mfupi kabla ya kuondoka nchini juzi kurejea Ubelgiji, Lissu alisema msimamo wa CHADEMA ni kutotambua uchaguzi na kwamba hawawezi kukubali nafasi za wabunge wa viti maalum walizopewa.

"Tumesema katika vikao vya kamati kuu ambavyo ni halali kwamba huu haukuwa uchaguzi, hatuwezi kushiriki kuhalalisha haramu na kuchukua viti maalum tulivyopewa kutokana na huo uharamu, ni kuhalalisha uharamu,"alisema Lissu.

Kuhusu orodha ya wabunge wateule wa chama wa viti maalum kupelekwa Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), Lissu alisema:

"Sheria ya Uchaguzi inasema orodha ya wagombea wa chama inapelekwa na Katibu Mkuu wa chama, wanaweza kufanya lolote wanalofanya, lakini halitakuwa halali, ya haramu itabaki kuwa haramu."

Juzi, Katibu Mkuu wa CHADEMA, John Mnyika, alisema hajapeleka majina ya viti maalum NEC.

"Atakayechukua kiti kwa utaratibu wowote nje ya utaratibu uliowekwa na sheria, atakuwa anafanya uharamu, atakayelipwa fedha yoyote kutokana na viti maalum, atakuwa ni haramu, haramu haizai halali hata siku moja," alisisitiza.

Lissu alisema licha ya kuondoka nchini, bado mapambano yanaendelea kwa kuwa maisha yake ni ya mapambano.

"Hakuna shaka yoyote kwamba kuna kuunga juhudi, kuogopa, bali mapambano yataendelea," alisema.

Lissu alisema haendi uhamishoni bali ana haki ya kuishi Ubelgiji ambako aliishi kwa miaka mitatu akipata matibabu, akiahidi kurudi nchini baadaye kuendeleza kile alichokiita mapambano.

Kuhusu kesi zake na ruhusa ya serikali kuondoka, Lissu alisema: "Sijawahi kusikia ninatakiwa kuwa na ruhusa ya serikali kuondoka nchini, kesi sita zilizopo mahakamani sijawahi kupata amri ya mojawapo kuwa nikitaka kuondoka nchini niombe ruhusa ya mahakama.

"Nimeandika barua kwa hakimu kumjulisha kuwa ninaondoka, hivyo kesi itakapokuja nitakuwa sipo, nimemwambia ninaenda kwenye matibabu, ninaenda kuonana na madaktari wangu.

"Sijakimbia bali kuna vitisho dhidi ya usalama wangu. Ili nipambane, ninahitaji kuwa hai na siku zote wafu hawazungumzi, hawapambani, ninataka niwe salama ili tujipange upya kuendeleza mapambano."

Kwa mujibu wa NEC, CHADEMA imepata nafasi 19 za wabunge wa viti maalum, huku Chama Cha Mapinduzi (CCM) kikipata viti 94.

Katika uchaguzi wa Oktoba 28 mwaka huu, Rais John Magufuli alipata ushindi wa kura zaidi ya milioni 12 akifuatwa na Lissu aliyepigiwa kura milioni 1.9.

# Tanga Cement yataja kiini bei saruji kupanda

**Na Mwandishi Wetu**

KUPANDA kwa bei ya saruji nchini, kunatokana na wafanyabiashara wanaotaka faida kubwa ndani ya muda mfupi, kuiuza bidhaa hiyo kwa ulanguzi.

Mtendaji Mkazi wa Tanga Cement PLC, Ben Lema, alitoa kauli hiyo jijini Dar es Salaam juzi, akibainisha kuwa kiwanda hicho hakijapandisha bei ya saruji.

"Kwa sasa hatujapandisha bei za saruji ila mpango upo wa kufanya hivyo Januari mwakani ili kusaidia wanahisa kupata gawio lao," Lema alisema.

Alisema chanzo kimojawapo kinachosababisha bei ya saruji kupanda ni wauzaji wa rejareja ambao wamekuwa wakinunua saruji na kuuza kwa bei ya kulangua.

Alisema kipindi cha baa la corona, Tanga Cement PLC ilipata mahitaji makubwa ya saruji ambapo uzalishaji ulifikia tani 108,000 kwa mwezi Oktoba kutoka tani 95,000 hadi 98,000 kwa mwezi ilivyokuwa awali.

Mtendaji huyo alisema kiwanda chao kinazalisha kiasi cha tani 1,250,000 hadi 1,260,000 za saruji kwa mwaka.

Lema alibainisha kuwa kiwanda hicho kwa sasa kinasafirisha saruji yake kwa mikoa ya Kanda ya Kaskazini kwa kutumia treni ya mizigo iliyozinduliwa jijini Arusha hivi karibuni baada ya kutotumika kwa takribani miaka 30.

Alisema kutokana na mahitaji makubwa ya saruji kwenye soko nchini, wanajipanga kuwekeza katika ujenzi wa kiwanda kingine.

Alitumia nafasi hiyo kuikumbusha serikali kufanikisha mazungumzo yao ya awali juu ya uwekezaji wa ujenzi wa kiwanda cha uzalishaji saruji mkoani Arusha.

Mtendaji huyo alisema kampuni yake ina mpango wa kuongeza uzalishaji, lakini inasubiri mazungumzo ya awali baina yake na serikali juu ya uwekezaji huo.

Lema alisema mradi wa ujenzi wa kiwanda hicho ukitekelezwa, utasaidia kuzalishwa kwa tani 500,000 hadi 750,000 kwa mwaka.

Alisema ujenzi wa kiwanda hicho utachochea fursa za ajira na biashara kwa wananchi na kuchangia pato la taifa.

"Bado tuko kwenye mazungumzo na serikali juu ya mradi wa ujenzi wa kiwanda kipya cha saruji jijini Arusha kitakachosogeza huduma karibu zaidi kwa wananchi wa Kanda ya Kaskazini na maeneo mengine ya jirani," alisema.

Lema alibainisha kuwa mazungumzo haya yalianza mwaka 2016, akisisitiza: "Tunataka kuendelea kumuunga mkono Rais John Magufuli juu ya azma ya Tanzania ya viwanda."

# HESLB yatoa orodha itakaowapa mikopo

**Na Halfani Chusi**

BODI ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB), jana imetangaza orodha ya kwanza ya wanafunzi waliopangiwa mikopo kwa mwaka wa masomo 2020-2021 unaotarajia kuanza wiki ijayo.

Mkurugenzi Mtendaji wa bodi hiyo, Abdulrazaq Badru (pichani), katika mkutano wake na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, alitangaza neema hiyo, akibainisha kuwa Sh. bilioni 153 zimetengwa kuwafikia wanafunzi 47,000.

Alibainisha kuwa, kati ya wanufaika hao, wanaume ni 26,000, sawa na asilimia 57 na wanawake ni 20,341.

Badru alisema tayari bodi hiyo imeanza kupeleka fedha za wanafunzi waliopangiwa mikopo katika vyuo mbalimbali na kuwataka wanafunzi kupata taarifa zao kupitia akaunti walizotumia kuomba mikopo, maarufu SIPA, na kujiandaa kwenda vyuoni kwa ajili ya usajili.


"Serikali imeshatupatia fedha na tumeanza kuzipeleka vyuoni, lengo letu ni kuhakikisha wanafunzi wenye sifa, wanazikuta fedha vyuoni ambako watajisajili na kupokea ili watimize ndoto zao," alisema.

Mkurugenzi huyo alibainisha kuwa orodha ya pili inatarajiwa kutolewa Jumamosi ya wiki hii baada ya kukamilisha uchambuzi wa maombi unaondelea.

"Kwa hiyo, niwatake waombaji wa mikopo kuendelea kutembelea akaunti walizotumia kuomba, kupata taarifa kuhusu maombi yao," Badru alisema.

Katika mkutano huo, mkurugenzi huyo alisema wanafunzi wenye mikopo wanaoendelea na masomo katika vyuo mbalimbali nchini wapatao 44,629, pia wamepangiwa mkopo wenye thamnai ya Sh. bilioni 155.06.

" Wanafunzi wawa 44,629 wamepangiwa mikopo baada ya bodi kupokea matokeo ya mitihani yanayothibitisha kuwa mwanafunzi amefaulu kuendelea na masomo katika mwaka unaoanza na bado tunaendela kupokea matokeo ya wanafunzi waliokuwa na mikopo mwaka wa masomo uliopita na watapangiwa mikopo," alifafanua.



# Wahukumiwa kunyongwa hadi kufa kosa kuua kwa kukusudia

**Na Samson Chacha,** TARIME

WAKAZI watano, kati yao ndugu wawili wa wilaya za Tarime na Rorya, mkoani Mara, waliokuwa wakikabiliwa na kesi za mauaji wamehukumiwa kunyongwa hadi kufa baada ya kupatikana na hatia ya kuua kwa kukusudia.

Waliohukumiwa ni Chacha Nyaitati, Wolder Kaler, Ongoro Onyango, Bwana Onyando na Denis Ondigo.

Wakisomewa hukumu hiyo mwishoni mwa wiki na Jaji John Kahozya wa Mahakama Kuu Kanda ya Musoma, mshtakiwa Nyaitati, alipatikana na hatia ya kumuua Chacha Makuri, kwa kumkata panga shingoni na kusababisha kifo chake papo hapo wakati wakigombea ardhi.

Wengine waliohukumiwa ni Kaler na wenzake Onyando na Bwana Onyando, mtu na ndugu, waliopatikana na hatia ya kumkata mapanga na marungu Joshua Okumu, wakimtuhumu kwa wizi wa mifugo. Pia, Denis Ondigo, alipatikana na hatia ya kumuua mtoto wake wa kambo, Mass Daniel kwa kumpiga na fimbo kichwani.

Awali, Mwanasheria wa Serikali, Yess Temba, alidai kuwa mshtakiwa Nyaitati, alimuua Chacha Keny, Januari 21, 2019 katika kiwanja cha kujenga nyumba kwa madai ya mgogoro wa kugombea ardhi na Keny aliyekuwa na mafundi kwenye kiwanja hicho na mshtakiwa alimvamia na kumkata kwa panga shingoni na kusababisha kifo chake papo hapo.

Katika tukio la mauaji ya Okumu lilitokea Januari 21, 2019 na washtakiwa Kaler na wenzake kina Onyando, walikwenda nyumbani kwa Okumu huku wakiwa na silaha za jadi na kumchukua wakimtuhumu kwa wizi wa mifugo na walipofika porini walimkata mapanga na kusababisha kifo chake.

Pia, alidai katika tukio la mauaji ya Mass, aliuawa na baba yake wa kambo, Ondigo kwa kumpiga na fimbo kichwani, kabla ya mauaji hayo, mtoto huyo alikuwa amebakwa siku tatu kabla ya kufariki.

Wakili huyo wa Serikali, aliiomba mahakama hiyo kutoa adhabu kali kwa watuhumiwa kwa kusababisha vifo ili iwe fundisho kwa watu wengine wanaojichukulia sheria mikononi.

Jaji Kahozya, alisema ushahidi uliotolewa na upande wa mashtaka, unawatia hatiani watuhumiwa hao na kuwahukumu adhabu ya kunyongwa hadi kufa ili iwe fundisho kwa watu wengine.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

**TAASISI YA TEKNOLOJIA YA UJENZI**
***(THE INSTITUTE OF CONSTRUCTION TECHNOLOGY- ICoT)***

**TANGAZO NAFASI ZA MASOMO KWA MWAKA WA MASOMO 2020/21**

**1. UTANGULIZI**

Wizara ya Ujenzi Uchukuzi na Mawasiliano (Ujenzi) imeanzisha Taasisi ya Teknolojia ya Ujenzi *(Institute of Construction Technology – ICoT)* iliyosajiliwa na NACTE kwa namba ya usajili **REG/SAT/035P.** Taasisi hii imeanzishwa kwa kuunganisha kilichokuwa chuo cha Ujenzi Morogoro (MWTI) na Chuo cha Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi (ATTI) Mbeya vilivyokuwepo chini ya Wizara ya Ujenzi Uchukuzi na Mawasiliano (Ujenzi). Makao Makuu ya Taasisi hii (Main Campus) yatakuwa Morogoro kilipokuwa Chuo cha Ujenzi (MWTI) na kutakuwa na Tawi (Campus) ya Mbeya kilipokuwa Chuo cha ATTI – Mbeya.

**2. LENGO LA KUANZISHA TAASISI**

Uanzishwaji wa Taasisi hii unaendana na malengo ya Serikali ya kufikia Uchumi wa Kati ifikapo mwaka 2025 na nchi ya uchumi wa viwanda ambapo Sekta ya Ujenzi ni mdau muhimu katika kusaidia nchi kufikia malengo hayo. Hivyo, ili kufikia malengo hayo Tanzania inatakiwa kuwa na wataalam wa kutosha katika Sekta ya ujenzi katika ngazi za chini (artisans), kati (technicians) na wa juu (engineers). Aidha, hatua za Serikali zinaenda sambamba na malengo ya Sera ya Ujenzi ya mwaka 2003 inayosisitiza na kuhakikisha kuwa wataalam waliopo wanajengewa uwezo wa kitaalam katika ufundi ili kuendana na hali ya sasa ya ukuaji wa sayansi na teknolojia. Hii itawezesha kukabiliana na ushindani na kupata thamani halisi ya fedha zinazopelekwa kwenye utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

**3. KOZI ZINAZOTOLEWA**

| NA. | AINA YA MAFUNZO | SIFA ZA KUJIUNGA | MUDA WA MAFUNZO |
|---|---|---|---|
| 1 | Basic Technician Certificate - NTA Level 4 - Civil Engineering | Mwombaji awe na ufaulu unaoanzia alama "D" katika masomo ya Hisabati, Fizikia au *Engineering Science*, Kiingereza na somo lingine moja isipokuwa masomo ya dini kwa ngazi ya kidato cha nne au Cheti cha Ufundi Stadi (VETA) Level 3 kikiambatana na ufaulu wa kuanzia alama "D" katika masomo mawili kwa ngazi ya kidato cha nne. | Mwaka mmoja (1) |
| 2 | Basic Technician Certificate - NTA Level 4 - Electrical Engineering | | |
| 3 | Basic Technician Certificate - NTA Level 4 - Mechanical Engineering | | |

**4. ADA**

Ada zetu ni nafuu na zitalipwa kwa awamu moja au mbili kulingana na uwezo wa mwanafunzi. Pia, Chuo kinatoa huduma za hostel kwa wanafunzi watakao wahi. Maelezo mengine yanapatikana katika masharti ya udahili yanayopatikana Chuoni au kupitia mawasiliano yaliyotolewa hapo juu.

**5. MAELEZO YA KUJIUNGA NA CHUO**

- **Waombaji wote wenye sifa wanapaswa kuwasilisha maombi yao kwa:**

**Mkuu wa Chuo,**
**Taasisi ya Teknolojia ya Ujenzi (ICoT), S.L.P. 963,**
**MOROGORO.**
**Tel. +255 23 2614098**
**Fax +255 23 2935227**

- **Fomu za kujiunga na Chuo zinapatikana kwa Mkuu wa Chuo, Morogoro simu +255 23 2614098/ 0685541188, ATTI - Mbeya simu namba 0784500738 na Makao Makuu ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano (Ujenzi) - Dodoma simu namba +255 26 2324455 / 0713815110 / 0712607291. Fomu hizi pia zinapatikana katika Tovuti ya Wizara ambayo ni www.mwtc.go.tz.**

- **Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 20 Novemba, 2020.**

***Wahi ili upate nafasi katika chuo chetu ambacho ni miongoni mwa vyuo vichache vya Serikali ya Tanzania vinavyofundisha fani hizi kwa vitendo zaidi.***

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Wanasiasa vumilianeni

**WABUNGE** wamekula kiapo na sasa jukumu lililo mbele yao ni kuishauri, kuisimamia na kuikosoa serikali bila kusahau kujadili na kupitisha bajeti.

Tunawakumbusha kuwa kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ibara ya 20(1) kila raia anastahili kuwa huru bila ya kuathiri sheria za nchi kukutana na watu wengine kwa hiari yake na kwa amani, kuchanganyika na kushirikiana na watu wengine, kutoa mawazo hadharani na hasa zaidi kuanzisha au kujiunga na vyama au mashirika yaliyoanzishwa kwa madhumuni ya kuhifadhi au kuendeleza imani au maslahi yake au maslahi ya wengine.

Kwa hiyo hakuna sababu ya kuendeleza uhasama wa kivyama tena iwe nje na ndani ya bunge kwani si kosa Mtanzania kuwa mwanachama anachokitaka. Hata wale waliohama chama na kujiunga na CCM na sasa ni wabunge hawajavunja sheria za nchi na taratibu zake ni sahihi kabisa kwa mujibu wa sheria na katiba.

Hivyo hatutarajii kuona tena uhasama ukiendelea iwe ndani au nje.

Ni wazi kuwa hakuna tatizo kila mmoja kufanya jambo analolipenda hata kama ni kutafuta maslahi yake binafsi au ya wengine iwe kwenye siasa au biashara na pengine popote.

Hivyo, tunawaomba wanasiasa kuwa na uvumilivu wa kisiasa na waepuke kulaumiana kwa kuwa kuna maisha baada ya uchaguzi na kula kiapo cha utii cha mbunge.

Uvumilivu wa kisiasa ndiyo pekee utakowafanya wale wasiokuwa na wabunge kuamini kuwa hawakufanya kosa kwa mujibu wa sheria na katiba, aidha, watakuwa na mipango mingine ya kuwapeleka kwenye uchaguzi mpya wa 2025 wakiwa na vyama vyenye nguvu na matumaini mapya.

Tunafahamu kuwa uchaguzi wa mwaka huu 2020 umehitimishwa na pengine wapo wengi ambao wanapata majeraha kisiasa kama kupoteza maisha, kujeruhiwa na mali zao kuharibiwa kama wanasiasa wema si vibaya kuamua kuyajadili na kuyamaliza kwa utaratibu badala ya kuendeleza mikwaruzano na chuki zinazosababisha wengine kuondoka nchini, wakidai kuwa maisha yao yako hatarini.

Ni vyema wanasiasa na vyama kufahamu kuwa hakuna taasisi duniani yenye watu wenye akili timamu inayoweza kuendeshwa bila kutofautiana katika mitazamo na fikra, na hili ni jambo la kawaida na hivyo inathibitisha kuwa akili ni nywele kila mtu ana zake na pia kila mmoja ana haki ya kuwa na maoni na misimamo yake.

Hata hivyo, kama hakuna kutofautiana kwenye kufikiri na kuamua mambo mbalimbali, ni wazi hakutakuwa na mitizamo tofauti hivyo, wanasiasa wafahamu kuwa hakuna siku watafanana mitazamo na fikra, kwa hiyo ni lazima wavumiliane.

Kwa hivyo kugombana na kulumbana kuhusu uchaguzi uliomalizika na hata kutishiana maisha kwa sababu ya kutofautiana kwenye kufikiria na kuamua si suluhisho la matatizo yenu.

Wanasiasa wa upinzani wafahamu kuwa cha msingi ni kuendelea kujadiliana na serikali na wadau kuhusu kuwapo kwa Tume Huru ya Uchaguzi ambayo kila upande utaona kuwa inafanikisha malengo ya kukuza na kuendeleza demokrasia.

Kwa upande mwingine, tunaamini kwamba baada ya wabunge walioshinda kuapa, watatekeleza vyema jukumu lake la kuisimamia, kuikosoa na kuishauri serikali.

Ni dhahiri kwamba wabunge wengi wanatoka chama tawala, lakini hilo lisiwafanye wakashindwa kutekeleza jukumu lao kwa mujibu wa katiba kama mhimili wa kutunga sheria na kuisimamia serikali.

Tunatarajia kuwaona wakiiuliza maswali serikali na kuihoji bila woga kuhusiana na mambo ambayo watabaini hayaendi sawa.

Matarajio yetu hayo yanatokana na kauli aliyoitoa Spika wa Bunge, Job Ndugai, kwamba Watanzania wasidhani kuwa bunge hilo litakuwa la 'Sawa Mzee'. Kwa upande wake, Rais John Magufuli akizungumza na wabunge wa CCM jijini Dodoma, aliwataka kuikosoa serikali bila woga ingawa aliwataka wasivuke mipaka.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Tusijisahau, magonjwa yasiyoambukiza yanaondoka na theluthi ya uhai wetu

Na Sabato Kasika

**MAGONJWA** yasiyoambukiza yanatajwa na wataalamu wa afya kuwa hayahami kutoka kwa mtu moja hadi mwingine, kwa vile hakuna vimelea katika mwili wa binadamu, ambavyo vinahusiana na magonjwa hayo.

Pia, yanatajwa kuwa magonjwa yanayozuilika, iwapo kila mtu atachukua tahadhari mapema kwa kuzingatia ulaji bora, kupunguza ulevi usiofaa, kupunguza uvutaji wa sigara na kuzingatia mambo yote muhimu.

Baadhi ya magonjwa yasiyoambukiza yanatajwa kuwa ni maradhi ya moyo, kisukari, saratani, magonjwa ya njia ya hewa, selimundu, yanayosababishwa na ajali, figo, akili, dawa za kulevya na magonjwa sugu ya meno na macho.

Mbali na kusababisha maisha ya watu kufupishwa, ni chanzo cha hasara kitaifa, kwa kuondoa nguvukazi ya umma na inarudisha nyuma maendeleo ya mtu binafsi na taifa kwa ujumla.

Aidha, yanaongeza mzigo kwenye mfumo wa afya kwa kuwa ni magonjwa ya muda mrefu na yanatumia rasilimali nyingi.

Anarejea takwimu za mwaka 2017, yamesababisha asilimia 33 ya vifo vyote nchini.

Tayari kuna jumla ya vifo 134,600 vilivyoripotiwa kuhusiana na magonjwa yasiyoambukiza, vilevile vitokanavyo na magonjwa ya moyo vikichukua kwa asilimia 13.

Vifo vya maradhi mengine na kiwango cha asilimia zake katika mabano ni: Kisukari (2), saratani (7), ajali (11) hali ambayo analalamika haikubaliki, hivyo kuna haja ya kujitathmini kupanga mikakati ya kukabiliana nayo.

Mganga Mkuu wa Serikali, Prof. Abel Makubi, analiambia Kongamano la Pili la Kitaifa la Kisayansi la Magonjwa Yasiyoambukiza, wiki hii jijini Dar es Salaam.

Anasema katika mwendelezo wa Maadhimisho ya Wiki ya Kuzuia na Kudhibiti Magonjwa Yasiyoambukiza, ni muhimu kutafakari na kuchukua hatua kulingana na kile ambacho wataalamu wa afya wanaelekeza.

Prof. Makubi, anazitaja takwimu za Shirika la Afya Duniani (WHO) kwamba, magonjwa yasiyoambukiza yanachangia zaidi ya vifo milioni 41, ambayo ni sawa na asilimia 71 ya vifo vyote milioni 57 vilivyotokea mwaka 2016.

Hiyo maana yake katika kiwango cha dunia, ni kwamba yanachangia zaidi ya robo tatu ya vifo ambavyo kama ugonjwa ungetambulika mapema, vingeweza kuepukwa na waathirika wakuu, mataifa ya uchumi wa kati ikiwamo Tanzania.

Muungwana anaamini kwamba, serikali imekuwa ikitoa elimu ya kutosha ya namna bora ya kukabiliana na magonjwa hayo, hivyo ni wajibu wa kila Mtanzania kuzingatia katika jitahada za kutetea na kuokoa maisha yake.

Hapo kuna muhimu wa ulaji bora, kupunguza ulevi na uvutaji sigara, pia kuzingatia michezo, kwani ni muhimu kwa kila mmoja anayetaka kuhakikisha afya yake inakuwa salama.

Kwa ujumla ni kwamba, kubadili tabia na mwenendo wa ulaji wa vyakula kwa kuongeza ulaji wa mboga za majani, matunda na kudhibiti matumizi ya vilevi ni njia rahisi ya kuepuka magonjwa yasiyoambukiza.

Umefika wakati, sekta zote nchini zikashirikishwa katika kudhibiti magonjwa yasiyoambukizwa, ili kuisaidia jamii kujiepusha na madhara yanayojitokeza, vivyo hivyo kupunguza gharama zinazojitokeza kwa matibabu.

Muungwana anaelewa kwamba, serikali ina jukumu la kuhakikisha huduma za afya zinaboreshwa kwa kujenga miundombinu ya msingi, kufanya utambuzi wa haraka wa magonjwa na kutoa tiba kwa wakati ili magonjwa hayo.

Niongeze, kuhusu umuhimu wa kushirikisha sekta mbalimbali katika kupunguza matatizo yanayosababishwa na magonjwa yasiyoambukiza, ili kila mmoja awe na jukumu la kulinda afya za jamii inayomzunguka.

Siyo vibaya serikali kupitia Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto wakachukua hatua ya kuwashirikisha wadau wengine wa kiserikali, wakiwamo mamlaka kama ya ardhi, mazingira, kilimo na wengine wakaungana kutoa elimu kwa umma.

Ni njia ikayosaidia kuushirikisha umma katika kupata elimu kikamilifu, kwa ajili ya kudhibiti magonjwa yasiyoambukiza ili kupunguza vifo vinavyotajwa kusababishwa na magonjwa hayo.

Niseme, hatua hiyo itasaidia pia kupunguza gharama kubwa katika kutafuta matibabu ya magonjwa yasiyoambukiza na badala yake elimu itakuwa msingi wa kuwasaidia kujikinga na magonjwa hayo.



Baadhi ya askari wa Jeshi la Polisi wakiwa kwenye maandalizi ya gwaride maalum katika viwanja vya Bunge, jijini Dodoma jana, kwa ajili ya kumpokea Rais Dk. John Magufuli, atakapolizindua rasmi Bunge kesho. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Mabalozi wakabidhi hati za utambulisho

**Asraji Mvungi, ARUSHA**

MABALOZI wawili wa Uingereza na Uswisi nchini, wamewasilisha hati za utambulisho wao kwa Katibu Mkuu wa Jumuiya ya Afrika ya Mashariki (EAC), Balozi Liberate Mfumukeko.

Hafla ya makabidhiano hayo ilifanyika jana jijini Arusha, ambako ni makao makuu ya EAC.

Waliowasilisha hati hizo ni Balozi David William (Uingereza) na Balozi Didier Chassot (Uswisi).

Akizungumza jana baada ya kupokea hati hizo, Katibu Mkuu wa EAC, Balozi Mfumukeko alisema: "Hizi ni nchi ambazo kwa muda mrefu zimekuwa na ushirikiano wa dhati na jumuiya yetu. "Tumezungumza mambo mengi yakiwamo yanayohusu hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa miradi mbalimbali inayoendelea kwa ushirikiano na nchi zao.

"Kimsingi, nimewaelezea maeneo ambayo bado tunahitaji kuongeza nguvu katika miradi inayoendelea kutekelezwa."

Katibu Mkuu wa EAC alizishukuru nchi hizo kwa ushirikiano na misaada mbalimbali kwa jumuiya hiyo.

Balozi wa Uingereza alisema amepokea taarifa ya Katibu Mkuu wa jumuiya hiyo inayoonyesha shughuli zinazofanywa kwa ushirikiano wa Uingereza na jumuiya hiyo.

Kutokana na ushirikiano huo, ameahidi kuendeela kutoa ushirikiano wa hali na mali katika kuhahakikisha miradi yote inayotekelezwa na EAC, inakuwa na tija na malengo yaliyowekwa yanatimia. Balozi Chassor wa Uswisi alieleza matumaini yake, akisema nia ya serikali ya nchi hiyo ni kuimarisha ushirikiano na nchi wanachama wa EAC.

# Wafungwa miaka 20 jela kwa kuwaingiza wahamiaji haramu

**Na Julieth Mkireri,** BAGAMOYO

MAHAKAMA ya Wilaya ya Bagamoyo mkoani Pwani, imewahukumu kifungo cha miaka 20 wakazi sita wa wilaya hiyo kwa kosa la kuwaingiza nchini wahamiaji toka Ethiopia kinyume cha sheria.

Mwendesha Mashataka wa Uhamiaji, Fadhili Msambwa, aliiambia mahakama hiyo kuwa watuhumiwa hao kwa kipindi kirefu, wamekuwa wakifanya biashara haramu ya kuingiza na kuwaficha wahamiaji kutoka Ethiopia.Akidai kuwa watuhumiwa hao wamekuwa wakiwasaidia wahamiaji hao kuwasafirisha kwenda Afrika Kusini hadi walipokamatwa mwezi uliopita.

Katika kesi hiyo ambayo illiyokuwa ikisikilizwa katika Mahakama ya Wilaya ya Bagamoyo na kuhamishiwa katika gereza la Kigongoni, mahakama pia imewahukumu kwenda jela miaka miwili kila mmoja, raia 259 kutoka Ethiopia baada ya kukutwa na kosa la kuingia nchini bila kibali.

Mkuu wa Idara ya Uhamiaji wa Mkoa wa Pwani, Naibu Kamishna wa Uhamiaji Paulo Eranga, ameishukuru mahakama hiyo kwa kutoa adhabu ambayo alisema itakuwa fundisho kwa Watanzania wengine wenye tabia kama hiyo.

# Vyuo vya maendeleo jamii vyaelekezwa

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

SERIKALI imewaagiza wakuu wa vyuo vya maendeleo ya jamii, kujipanga katika uongozi wa kimkakati utakaowezesha kutekeleza majukumu yao yatakayoleta mabadiliko chanya kwenye sekta hiyo na kufikia malengo yaliyokusudiwa.

Agizo hilo limetolewa na Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii,Jinsia,Wazee na Watoto-idara Kuu ya Maendeleo ya Jamii, Dk. John Jingu, kwenye kikao kazi elekezi cha mafunzo ya uongozi na tathmini kilichofanyika mkoani Morogoro.

Dk. Jingu alisema mkakati wa Serikali kwa sasa ni kuhakikisha vyuo hivyo vinakuwa chachu ya kuleta mabadiliko kulingana na sera, dira na miongozo inayotolewa na viongozi wa juu, hatua ambayo italeta maendeleo haraka.

"Ipo miongozo kutoka kwa viongozi wetu wa juu kuhusu mikakati ya kuleta maendeleo, hivyo ni lazima kujipanga upya nyinyi wakuu wa vyuo vyetu hivi ili kufikia malengo yaliyokusudiwa," alisema Jingu.

Aliwataka wakuu hao kusimamia kwa nguvu programu za vyuo vyote vya maendeleo ya jamii kuwa chachu ya kuleta mabadiliko kwa wananchi ili kufia malengo yaliyowekwa.

Mkurugenzi wa Maendeleo ya Jamii Idara Kuu ya Maendeleo ya Jamii, Patrick Gowike, alisema lengo la mafunzo hayo ni baada wizara kufanya mabadiliko hivi karibuni ya wakuu wa vyuo na makamu wao, hivyo ni lazima wapewe mafunzo ya uongozi ili kuleta tija kulingana na mahitaji ya sasa.

Alisema lengo la kufanyika kwa mabadiliko hayo ni wizara kuendelea kuzalisha maofisa maendeleo ya jamii kuzalisha watalaam mahiri waendane na soko la ajira pamoja na kuwa chachu ya kuleta maendeleo nchini.

# TBA yatamba kutekeleza ujenzi kwa viwango

**Na Richard Makore,**
MWANZA

WAKALA wa Majengo Tanzania (TBA), umesema utaendelea kutekeleza miradi mbalimbali ya ujenzi ya serikali mkoani Mwanza ili kuokoa fedha nyingi ambazo zingepotea kwa makandarasi binafsi.

Akizungumza na Nipashe ofisini kwake jana jijini hapa, Kaimu Meneja wa TBA Kanda ya Ziwa, Moses Urio, alisema miradi iliyopewa TBA na serikali imesimamiwa na baadhi imekamilika huku mingine ikiwa katika hatua za mwisho.

Urio alitaja baadhi ya miradi waliyopewa na serikali Kanda ya Ziwa kuwa ni pamoja na upanuzi wa Hospitali ya Rufani ya Mkoa ya Sekou Toure, jengo la Halmashauri ya Wilaya ya Misungwi, Ofisi za Mkuu wa Wilaya ya Nyamagana na makazi ya Mkuu wa Mkoa.

AlisemaTBA inafanya kazi katika wilaya zote za mkoa wa Mwanza na kwamba kwa kutumia watalaam wake na binafsi, inafanya kazi hizo kwa gharama nafuu ikilinganishwa na kampuni binafsi za ujenzi.

Kuhusu upangishaji wa zaidi ya nyumba 600 zilizoko Kanda ya Ziwa, Urio alisema wanakabiliwa na changamoto ya wapangaji kushindwa kulipa kodi kwa wakati.

Urio alisema wapangaji wengi wanashindwa kulipa kodi licha ya kuwa ni nafuu pamoja na baadhi yao kupangisha watu wengine wanapotaka kuondoka kwenye nyumba hizo.

"Nyumba zetu zimeenea mkoa wote wa Mwanza pamoja na wilaya zake na wapangaji wanaoshindwa kulipa. Tunatumia madalali wa mahakama kuwaondoa na kuweka watu wengine," alisema.

Aliongeza kuwa utaratibu wao unakataza mtu kupangisha ama kumrithisha mtu au ndugu na kwamba kila baada ya muda huwasaka watu wa namna hiyo.

Meneja huyo alisema watu wanaobainika kukiuka utaratibu wa kupangishwa nyumba hizo, huondolewa kinguvu na kuwapa wapangaji wengine waliofuata taratibu.




Mbunge wa Ukonga, Jerry Silaa (kushoto), akizungumza na maofisa wa Benki ya NMB katika viwanja vya Bunge mjini Dodoma jana.
**PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Coca-Cola yaipa kompyuta shule Dar

**Na Elizabeth Zaya**

KAMPUNI ya vinywaji baridi ya Coca-Cola kwanza Ltd, imetoa kompyuta kwa Shule ya Sekondari ya Mbezi Inn jijini Dar es Salaam, ili kuhamasisha ukuaji wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano katika kufundisha na kujifunzia, kuwezesha na kuandaa walimu na wanafunzi katika ulimwengu wa TEHAMA.

Akizungumza wakati wa mahafali ya 13 katika shule hiyo, Ofisa wa Masuala ya Umma na Mawasiliano wa Coca-Cola Kwanza, Victor Byemelwa, alisema sababu za kampuni hiyo kutoa msaada huo ni kuunga juhudi za serikali katika kukuza na kuboresha ujumuishaji wa TEHAMA katika sekta ya elimu.

Byemelwa alisema lengo la msaada huo wa Coca-Cola kwanza ni kuboresha tasnia ya elimu na kusaidia wanafunzi kujifunza na kukuza ujuzi wao kupitia ICT.

Alisema Kampuni hiyo imekuwa ikijihusisha mara kwa mara kusaidia serikali katika sekta ya elimu katika kutatua matatizo mbalimbali hususani katika eneo la uhaba wa madawati.

Alisema wamekuwa wakilazimika kutoa msaada huo ili kuhakikisha inatoa sehemu ya faida wanayoipata na kurudisha kwa jamii.

"Kampuni ya Coca-Cola Kwanza imetoa kompyuta ili kuwawezesha walimu, pamoja na viongozi wote wa shule hii kutumia TEHAMA kwa ufanisi katika shughuli zao za kila siku na kuongeza ubora wa elimu katika shule hii," alisema Byemelwa. Kwa upande wake, Mjumbe wa Bodi ya Shule hiyo, Varelian Komu, alisema tangu kufunguliwa kwa shule hiyo mwaka 2005, haikuwa ikifundisha masuala ya ICT kwa sababu ya ukosefu wa miundombinu na kwamba msaada huo umekuja kwa wakati muafaka na utasaidia kwa kiwango kikubwa shule hiyo kuanza kufundisha masuala hayo na kutoa wito kwa wadau mbalimbali kuendelea kusaidia kuinua sekta ya elimu nchini.

Akizungumzia kuhusu msaada huo, mmoja wa wanafunzi wa shule hiyo anayesoma kidato cha nne, Sylvia Julius, aliishukuru na kuipongeza kampuni ya Coca-Cola kwanza kwa kujitoa kuwasaidia vifaa hivyo.

Alisema wao kama wanafunzi wanaamini kwamba msaada huo utawapa chachu ya kujifunza masuala ya ICT na pia itawarahisishia katika ujifunzaji.

# Wakubaliana kusambaza umeme jua kwa bei nafuu

**Na Beatrice Shayo**

BENKI ya Equity imesaini mkataba na kampuni ya umeme wa jua ya Zola kwa ajili ya kusambaza nishati hiyo kwa gharama nafuu kwa lengo la kuwainua kiuchumi.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam, Mkurugenzi Mtendaji wa benki hiyo, Robert Kiboti, alisema lengo la kuingia makubaliano hayo ni kuwawezesha wateja wao kupata umeme jua hususani katika maeneo ya vijijini na mjini.

Alisema mteja atapatiwa mkopo wenye riba nafuu ili aweze kupatiwa nishati ya jua na kuutumia kwa saa 24 bila kulipa chochote.

"Tumejipanga kuwasaidia wateja wetu kutumia nishati hiyo ambayo inauzwa kwa gharama nafuu, ili waache kutumia nishati ambazo sio nzuri na zenye kuhatarisha usalama wa maisha yao hasa kwa vijijini," alisema Kiboti.

Kiboti alisema wateja wake wakiwa na umeme itawasaidia katika kuboresha maisha yao kiuchumi.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa Afrika Mashariki wa kampuni ya Zola, Johnson Kiwango, alisema walifanya utafiti wao na kubaini kuwapo na tatizo la gharama kubwa katika nishati ya jua.

Alisema lengo la kusaini mkataba huo ni kuwawezesha wananchi kupata sola yenye ubora na kwa gharama nafuu.

Kiwango alisema mteja anapopatiwa bidhaa feki inamrudisha nyuma kimaendeleo, hivyo wameamua kuleta nishati hiyo iwasaidie badala ya kuwakandamiza.

Alisema wana mitambo ya vijijini na mjini kwa ajili ya kusambaza umeme jua ili wananchi kuacha kutumia nishati za zamani kama mafuta ya taa ambayo sio salama.

Aidha, Kiwango alisema bado kuna maeneo mengi hayana umeme na kwamba watashirikiana na serikali katika kuwawezesha wananchi wanapata nishati hiyo.

Alisema nishati hiyo imesaidia katika maeneo ya vijijini na kuwa kuna baadhi walikuwa wanafunga biashara zao mapema kutokana na kukosekana kwa mwanga.

"Tulivyowafungia umeme jua kwa sasa wanafanya biashara hadi usiku kwa sababu wana uhakika wa umeme, na hata kipato kitaongezeka," alisema Kiwango.



Wanawake wa Mtaa wa Tabata Kisukuru, jijini Dar es Salaam, wakiwa wamepanga foleni ya kuchota maji kwenye kisima kifupi jana, kutokana na kukosekana kwa maji ya bomba kwa muda mrefu. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Mvua yaacha kilio kwa wafanyabiashara

**Na Richard Makore,** MWANZA

MVUA kubwa iliyonyesha siku nzima juzi, imeacha kilio kwa wafanyabiashara wa soko la samaki eneo la Kamanga jijini Mwanza, baada ya mafuriko kusomba majokofu wanayotumia kuuzia samaki.

Mafuriko hayo yamelisomba soko hilo maarufu la samaki la Kamanga na kusababisha hasara kwa wafanyabiashara hao.

Akizungumza na Nipashe katika eneo hilo, Makamu Mwenyekiti wa wafanyabiashara wa soko hilo, Raphael Magambo, alisema, licha ya wao kulipa ushuru, lakini wamekuwa wakifanya biashara katika mazingira mabaya.

Alisema eneo hilo linazungukwa na mitaro mikubwa inayoingiza maji katika Ziwa Victoria, na kwamba wakati wa mvua mafuriko huwakumba mara kwa mara. Magambo alisema licha ya kukumbwa na mafuriko, pia kipindi cha jua wanapata shida kwa sababu wamezuiwa kujenga kitu chochote katika eneo hilo. Aliongeza kuwa katika kipindi hiki cha mvua wanashindwa kufanya biashara kwa kuwa eneo lote linajaa maji na matope.

Kwa upande wake, mmoja wa wafanyabiashara katika eneo hilo, Silvia Bunoge, alimwomba Rais John Magufuli kuwasaidia eneo zuri la kufanyia biashara zao.

Alisema wanalipia leseni za biashara na ushuru mwingine wa serikali, lakini wameshindwa kusaidiwa kuboreshewa mazingira yao ili waweze kufanya biashara. Naye mfanyabiashara katika eneo hilo, Neema Wilson, alisema majokofu wanayotumia kuuzia samaki yalisombwa na maji na kwamba walifanya jitihada kuyaokoa yasiingie ziwani.

Alimwomba Rais Magufuli na viongozi wengine wa serikali mkoani humo, kuwasaidia wafanyabiashara hao sehemu za kufanyia biashara.

Mvua inaendelea kunyesha katika mkoa wa Mwanza na baadhi ya wilaya zake huku sehemu zingine zikikumbwa na mafuriko na wengine wakipata neema ya kulima mazao.

# Mtaalamu wa afya aiasa jamii magonjwa ya mlipuko

**Na Timothy Itembe,** TARIME

JAMII imeshauriwa kipindi hiki cha mvua za masika zinazoendelaea kunyesha kutibu maji kwa kutumia dawa zilizothibitishwa na Wizara ya Afya ili kujikinga na magonjwa ya mlipuko.

Ushauri huo ulitolewa mjini Tarime na Ofisa Afya na mratiba uelimishaji afya wa Halmashauri ya mji wa Tarime, Agrey Hyera, alipozungumza na vyombo vya habari.Agrey alisema kuna magonjwa ya mlipuko mengi nyakati za masika, hivyo jamii inatakiwa kuchukua tahadhari ya kujikinga kama vile kuchemsha maji na kuyachuja kwa matumizi ya nyumbani.

"Mimi kama mtaalamu wa afya, niseme kuwa jamii inakumbwa na magonjwa ya mlipuko kutokana na kutozingatia taratibu na kanuni za afya," alisema Agrey.

Aliwashauri Watanzania kuchukua tahadhari juu ya ugonjwa wa corona hususani wale ambao wanaishi mipakani kama Tarime jirani na Kenya, huku wakijua kuwa ugonjwa huu unaendelea kuwatesa watu wa mataifa mengine yakiwamo ya jirani na Tanzania.

Alibainisha kuwa baadhi ya magonjwa ya mlipuko ambayo yanatokea kipindi cha mvua ni kuhara, kipindupindu na magonjwa ya matumbo.

Mmoja wa wakazi wa mjini hapa, Faustena Jumanne, alibainisha kuwa wananchi wengi wa Tarime wamejenga tamaduni ya kutumia maji ya mvua bila kuyatibu, huku wakiamini kuwa yametoka kwa Mungu na ni salama.

Jumanne aliongeza kuwa bado elimu ya afya haijawafikia walio wengi hususani juu ya matumizi sahihi ya maji kwa matumizi ya nyumbani.

# Stanbic yatwaa Tuzo Benki Bora uwekezaji mwaka 2020

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya Stanbic Tanzania imeshinda tuzo ya Benki Bora ya Uwekezaji Tanzania kwa mwaka 2020, iliyotolewa na jarida la EMEA Finance Oktoba.

Jarida hilo linajishughulisha na kuripoti matukio kwenye sekta ya fedha ulimwenguni pamoja na kutambua benki zinazofanya vizuri katika vipengele mbali mbali.

Tuzo ya Benki Bora ya Uwekezaji inatolewa kwa kuangalia utaalamu wa benki husika katika masoko na ubora wa utoaji huduma kwa upande wa uwekezaji.

Akizungumzia tuzo hiyo, Mkurugenzi wa benki ya Stanbic Tanzania, Kevin Wingfield, alisema ushindi huo ni kielelezo cha namna benki hiyo imekuwa mstari wa mbele katika sekta ya uwekezaji nchini.

"Kwa miaka mingi, Stanbic imekuwa ikiunga mkono malengo ya serikali na wafanyabiashara wanaotafuta ubia na benki yenye uwezo wa kutoa huduma bora katika uwekezaji. Msingi wetu imara na uzoefu katika kutoa ushauri wa kitaalamu ndio umetuwezesha kutwaa tuzo hii," alisema Wingfield.

"Kwa miaka mingi tumekuwa tukishirikiana na wateja wetu kwenye miradi mbalimbali kama miundombinu, nishati, madini, mawasiliano, ujenzi na biashara, ambayo ni muhimu katika kuchochea ukuaji wa kiuchumi nchini," aliongeza Wingfield.

Wingfield aliongeza kuwa kutwaa tuzo hiyo ni matokeo ya jitihada za pamoja kati ya wateja na wabia wa benki hiyo, na benki inaahidi kuendelea kutengeneza huduma bunifu za kuwezesha ndoto mbalimbali kutimia kwa kuhakikisha ufanikishaji wa miradi nchini.

# Mil. 346/- kukarabati shule ya sekondari

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

KIASI cha Sh. milioni 346, kimetengwa kwa ajili ya kukarabati Shule ya Sekondari Mwadui Technical, iliyopo wilayani Kishapu mkoani Shinyanga.

Mkurugenzi Msaidizi wa Elimu Sekondari kutoka Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Benjamin Oganga, alibainisha hayo juzi alipofanya ziara ya kukagua ukarabati wa ujenzi wa madarasa, na mabweni katika shule hiyo.

Alisema shule hiyo ilijengwa mwaka 1997 chini ya mgodi wa almasi Mwadui, ambapo kwa sasa baadhi ya majengo yake yamechakaa na kuanza kutoa nyufa, hivyo lengo la kutengwa kiasi hicho cha fedha ni kuyafanyia ukarabati na kunusuru maisha ya wanafunzi wasije wakaangukiwa.

"Nakuomba sana mkuu wa shule hii, uzisimamie vizuri fedha hizi, ili ukarabati wa majengo haya ya madarasa na mabweni yawe imara, na fedha zitakazobaki zitumike kupaka rangi shule nzima na ipendeze," alisema Oganga.

Naye Mkuu wa Shule hiyo, Shija Dominic, aliishukuru serikali kuifanyia ukarabati na kubainisha kuwa wanafunzi walikuwa wakisoma kwa wasiwasi wakihofia kuangukiwa na majengo, kutokana na kuona nyufa.

# Vibanda vya Magufuli kukamilika mwezi huu

**Na Frank Kaundula,** MOROGORO

ZAIDI ya wafanyabiashara 100 wa Kijiji cha Magole wilayani Kilosa Mkoa wa Morogoro, wanatarajia kunufaika na ujenzi wa mradi wa vibanda ambavyo ni agizo la Rais Magufuli alililolitoa miezi kadhaa iliyopita baada ya ujenzi kukamilika.

Hayo yalisemwa juzi na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Kilosa, Asajile Mwambambale, na kufafanua kuwa ujenzi wa vibanda hivyo ni agizo la Rais Magufuli alilolitoa Agosti mwaka huu, na kwamba ujenzi wake huo umekamilika.

"Mambo yakienda hivi bila shaka ujenzi utakamilika mwishoni mwa mwezi huu, hivyo wafanyabiashara wa Magole Wilaya ya Kilosa wajiandae kufanya biashara zao katika mazingira ambayo ni rafiki kwa shughuli zao," alisema Mwambambale.

Alisema ujenzi wa vibanda hivyo umeghalimu Sh. milioni 100, ambazo zilitolewa na Rais Magufuli aliposimama eneo hilo ambalo ni maarufu kwa biashara ya mahidi ya kuchoma, mabichi, mboga na mazao ya viungo.

Mwambambale alisema vibanda hivyo ni 14 ambavyo vina jumla ya vyumba 42, na kwamba ugawaji wake utazingatia matumizi jumuishi kwa wanyabiashara na hakutakuwa na upendeleo wa aina yoyote kwenye ugawaji.

Mkurugenzi huo alisema ujenzi wa mradi huo utaongeza mapato ya halmashauri yake, hivyo aliwataka wafanyabiashara watakaopata vibanda hivyo wavitumie kama fursa ya kujiongezea kipato.

Aidha, aliwataka wafanyabiashara hao kuvithamini na kuvitunza vibanda hivyo, pia aliwataka kumpa ushirikiano Rais Magufuli katika majukumu yake ya kuiongoza serikali kwani vibanda hivyo vimejendwa na kutoka na agizo lake.

Wafanyabiashara walimpongeza Rais Magufuli kwa kuwajengea eneo la kudumu la kufanyia biashara zao, na kueleza kwamba kuwapo wa eneo hilo ni fursa kubwa kwao ya kujinyanyua kiuchumi.

Ester Mbasha, alisema ujenzi wa vibanda hivyo utaongeza fursa nyingi za kibiashara katika eneo hilo, na kwamba kupitia shughuli zitakazofanyika mapato ya halmashauri yatapatikana.

Naye Sam Nyange, aliwataka wafanya biashara wenzake kuwa waaminifu katika suala zima la ulipaji ushuru wa serikali kwa maslahi ya taifa na pia kuzingatia usafi ili kuepukana na magonjwa ya milipuko hasa wakati wa mvua za masika.

# Wanafunzi kidato pili, tatu vinara kwa mimba

**Na Yasmine Protace,**
DODOMA

IMEBAINIKA kuwa wanafunzi walio na umri wa miaka 15 hadi 16, wanaosoma kidato cha pili na tatu, ni miongoni mwa wanaopata mimba za utotoni.

Hayo yamesemwa na Zawadi Bakari, askari kutoka Kituo cha Kati Polisi Dodoma katika dawati la jinsia.

"Kesi zinazokuja kwetu ambazo zinaongoza kwa kuripotiwa ni kesi za mimba, zimeshika nafasi huku zikifuatiwa na kesi za ukatili wa kijinsia," alisema.

Aliongeza kuwa katika kesi hizo za mimba, wengi wao ni wanafunzi wenye umri wa miaka 15 hadi 16 na wanasoma kidato cha pili na tatu. Akizungumzia jinsi wanavyofanya kazi na Shirika lisilo la kiserikali la Restless Development, alisema kuwa wanafanya kazi nalo vizuri na limeleta mchango mkubwa kwa kutoa elimu ambayo imewasaidia watu kufunguka pale wanapofanyiwa ukatili.

"Jamii awali ilikuwa haitoi taarifa inapofanyiwa matukio ya kikatili na hata kutoa taarifa watoto wanapokatiza masomo kwa kupata ujauzito, lakini baada ya kuanzishwa mradi wa Timiza Ahadi, ulioletwa na Restless, jamii imepata mafunzo na wameweza kujitambua," alisema Zawadi.

Aliongeza kuwa hata wanaume nao wamekuwa wakifika kutoa taarifa katika dawati pale wanapofanyiwa ukatili.

Kwa mujibu wa Zawadi, likizo ya ugonjwa wa corona nayo haikuwaacha salama wanafunzi, kwa kuwa baadhi yao walipata mimba. Aliongeza kuwa changamoto wanayokumbana nayo ni baadhiya madaktari kujivuta kutoa ushahidi kesi za ukatili, mimba za utotoni na ubakaji.

Alibainisha kwamba hali hiyo, inachangia kuahirishwa kwa kesi na wakati mwingine kuchelewa kutolewa uamuzi



Mafundi wakijenga mfereji wa maji ya mvua katika kituo cha mabasi ya mikoani na nchi jirani, jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Watapishaji vyoo wakati wa masika wapewa onyo

**Na Mwandishi Wetu**

BARAZA la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) kwa kushirikiana na maofisa mazingira wa majiji, manispaa na halmashauri zote, wamejipanga kudhibiti watu wenye tabia ya kutapisha vyoo hasa katika kipindi hiki cha msimu wa mvua.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, Mkurugenzi Mkuu wa NEMC, Dk. Samuel Gwamaka, amesema baraza halitakuwa na huruma wala kurudishwa nyuma na watu wachache ambao wamekuwa kikwazo katika kulinda na kutunza mazingira.

"Hivi karibuni mtakumbuka kuwa nchi yetu imeingia katika uchumi wa kati na hiyo imetokana na jitihada mbalimbali zilizochukuliwa na serikali katika nyanja ya uchumi, afya, mazingira na sekta zingine. Hatutaki kurudi tena zama za kipindupindu hasa katika Jiji la Dar es Salaam," alisema Dk. Gwamaka.

Katika kuhakikisha wanadhibiti hali ya utapishaji, Dk. Gwamaka alisema baraza limejipanga kushirikiana na maofisa mazingira wa majiji, manispaa na halmashauri kudhibiti hali hiyo sambamba na kuwachukulia hatua kali za kisheria wahusika wote.

Dk. Gwamaka aliwaomba Watanzania kuendelea kushirikiana na NEMC hususani kupitia kitengo chake cha timu ya dharura, ambacho kinafanya kazi kwa saa 24 kila siku kwani mafanikio makubwa yamesha-patikana.

"Wito wangu kwa Watanzania wasichoke kutoa ushirikiano kwa baraza hasa kwa kitengo chetu cha dharura ambacho kimekuwa kikifanya kazi nzuri kwa saa 24, ili kukabiliana na changamoto za mazingira kwa kuwa watumishi wa chombo hicho hawawezi kuwa kila mahali," alisema.

Aidha, aliwashauri Watanzania kuunganisha nguvu ya pamoja kama wanadhani gharama za kutumia magari ya taka ni kubwa ili kuepuka adhabu kali ikiwamo kufikishwa mahakamani kwa sababu ya upishaji wa majitaka na utapishaji vyoo.

"Kuna taarifa tunazipata kutoka kwa watu mbalimbali kuwa changamoto inayochangia watu kutapisha vyoo ni gharama za ukodishaji magari ya taka ambayo yamekuwa yakinyonya majitaka katika makazi ya watu.

Nawashauri kuunganisha nguvu ya watu wawili au watatu, ili waweze kupata gari ambayo itanyonya majitaka kuliko kuyatiririsha kwenye makazi ya watu kinyume na sheria ya mazingira," alieleza.

ama

ALHAMISI NOVEMBA 12, 2020

AFYA NA MAZINGIRA



Ukurasa 13

**Miaka 13 maisha yahamia hospitalini hajiwezi, vidonda, mke naye ayeyuka**



Ukurasa 12

Namna ugonjwa macho unavyotesa watu



Ukurasa 14

**Kuugua Trump na alivyopona haraka, darasa la tiba wagonjwa corona wazee**

AFYA

MTAA KWA MTAA DODOMA...

# Tutimize Ahadi; mradi unaonusuru afya kwa kudhibiti ukatili wa jinsia

**Na Yasmine Protace,** Dodoma

HALI ya jamii kukosa mwamko sahihi, imekuwa fursa kwa jamii kufungua milango mateso katika yanayohusu kijinsia kuwaathiri, huku jamii ikiyafumbia macho.

Inaelezwa kwamba, katika jamii kuna hatua ambazo zimeshachukuliwa katika namna tofauti kukabili athari za kijinsia, pia upande wa pili kuna matukio ya kikatili yanapofanyika, kunadaiwa kuwapo dhana 'kumalizana juu kwa juu.'

Kuna baadhi ya maeneo ya kijamii kunakotajwa kuwapo hatua zilizokwishachukuliwa katika namna tofauti, hapo kukitajwa mradi uliokwishaanzishwa kujikita katika utekelezaji malengo ya vijana katika eneo hilo la ukatili wa kijinsia.

Amina Mhia, Wakili Mtetezi Uwajibikaji, kutoka kata ya Kikuyu Kaskazini, katika jiji la Dodoma, anasema matukio ya kesi za kijinsia yalikuwa mengi, ikiwamo ukatili kwa watoto.

Kuhusu ufuatiliaji wake, anasema walikuwa walipokutana na makundi ya vijana mbalimbali na waliwahoji kuhusu uelewa wao kuhusu masuala ya ukatili wa kijinsia na mimba za utotoni.

Amina anasema, vijana wengi walionekana kutozijua mimba za utotoni na waliomba kuelimishwa masuala yanayohusu huduma za uzazi, akiongeza hata sura ya matokeo chanya ni kwamba zahanati ya Kikuyu Kaskazini imejengwa kwa ajili ya huduma rafiki kwa vijana.

Kwa mujibu wa Amina, bajeti ya fedha za mradi inatekelezwa kwa ajili ya kuwasaidia kuhudumia marafiki na vijana, pia ushirikishaji umewasaidia kuelewa mengi yanayohusu mimba za utotoni na athari zake.

Wakili huyo anasema, ugumu wanaokutana nazo kazini kutekeleza mradi, sehemu mojawapo ni vijana waliogoma kubadiika, pale walipopatiwa elimu na wakaanza kujiamini.

Ni mafanikio kutoka hatua ya mpito ukatili ulipofanyika, utatuzi wake wanafamilia walikutana 'kumalizana wenyewe' pasipo kupitia kanuni za kisheria.

Anasema, hatua iliyofikia sasa ni kwamba elimu husika imeshazaa matunda, kwa wanaume wanapofanyiwa ukatili wa aina hiyo, nao wanaripoti katika mamlaka husika, wakitaka wahusika wachukuliwe hatua.

Johannes Thadeo, ni Wakili wa Uwajibikaji wa Vijana (YAA) katika mradi huo jijini hapa, anafanya kazi hiyo katika kata ya Chamwino, lengo kuu ni uhakikisha serikali inatimiza mkakati katika msauala ya ukatili wa kijinsia, ikiwamo uzazi wa mpango.

Anaongeza kwamba, mafunzo wanayoyatoa ni kwa jamii yameweza kuwasaidia wananchi na kuwawezesha kubadilika kwa kuwatoa sehemu fulani kwenda sehemu nyingine.

Thadeo anafafanua kwamba, watendaji wa kiserikali wamekuwa bega kwa bega nao katika kufanya kazi vizuri za huo mradi, pia kufanikisha kuandaliwa bajeti rafiki za uzazi kwa vijana.

Anasema, wameshafanya kazi na kuleta mafanikio makubwa kwa jamii, ambayo jamii imekwishafahamu athari za ukatili wa kijinsia na anajisifu kuwa mradi umeleta mafanikio makubwa kwa vijana wanaweza sasa kujitambua.

"Mradi unaitwa 'Tutimize Ahadi' na unatekelezwa kwa awamu mbili, ya kwanza ilianza mwaka 2018/2019, awamu ya pili ulianza mwaka 2019/2020," anasema.

Hadi sasa mradi huo unafadhiliwa na taasisi ya Bill and Melinda Gates Foundation ya Marekani na mradi huo ulitekelezwa na Restless Development, ukilenga kusimamia afya ya uzazi na usawa wa kijinsia .

Inaelezwa, katika jinsia wanatoa elimu ya masuala mbalimbali, ikiwamo ukatili dhidi ya watoto na unyanyasaji kijinsia na katika afya ya uzazi, vijana wa kiume hawakujua kama nao yanawagusa.

Ni ufafanuzi unaobainisha kwamba baada ya kujengwa uwezo, jamii ilijitambua kwamba suala la afya ya uzazi linagusa jinsia zote.

Vivyo, wanajamii wanasema katika masuala ya kikatili, walikuwa wanafumbia macho, lakini elimu waliopewa imewafumbua macho hata sasa wanatoa ushirikiano, pale matukio ya ukatili yanapofanyika.



Wakili wa Uwajibikaji, Amina Mahia, alipozungumza na waandishi wa habari (hawapo pichani) jijini Dodoma, siku chache zilizopita. **PICHA: YASMINE PROTUS**

**MAPUNGUFU**

Anataja kasoro zilizopo ni kushuhudia mwitikio mdogo kutoka kwa mabinti wanapoalikwa mafunzoni na kuna baadhi ya watu wanaotanguliza maslahi binafsi, huku kuna watendaji wanaonyima ushirikiano wanapohitaji takwimu. Kupata takwimu husika

Ofisa Mtendaji wa Kata ya Sokoni jijini hapa, Faraja Seki, anasema mradi huo umezaa matunda kwa wananchi kuweza kujua ufasaha kuhusu mimba za utotoni na ukatili kwa jumla.

AFYA

SIKU YA MACHO DUNIANI



Huduma za afya ya macho zikiendelea. **PICHA ZOTE: MPIGAPICHA WETU**

# Namna ugonjwa macho unavyotesa watu wengi

• Daktari: Tunapokosea ni kutelekeza ushauri bora

**Na Sabato Kasika**

MILANGO ya fahamu ni sehemu ya viungo vinavyomruhusu mtu kujua na kuyamudu mazingira yake kwa usahihi, ikiwa na milango mitano ya fahamu mwilini, kila moja na umuhimu wake.

Kazi ya macho ni kuona, masikio yanasikia, pua kazi yake kunusa, ulimi kazi yake ni kuonja na ngozi kazi yake kugusa.Yaani kila mlango una majukumu yake katika mwili.

Kibailolojia, kila kiungo kina uwezo kupokea habari za nje kutoka mwilini kama vile nuru, sauti, joto, mwendo, harufu na ladha, ili kuzibadilisha katika mfumo wa ki-umeme na kuchukuliwa njia ya mfumo wa 'neva' hadi ubongo.

Milango ya fahamu ni muhimu kwa binadamu kutokana na kusaidia kufanya shughuli za kila siku, hasa katika kufatuta mahitaji muhimu.

Ni mwezi uliopita yalifanyika maadhimisho ya Siku ya Afya ya Macho Duniani, yakiwa na yamebeba kaulimbiu isemayo "Afya ya Macho kwa wote, Matumaini ya Kuona" ikilenga kuwa na afya salama ya macho.

Lakini, kabla ya maadhimisho hayo ambayo kitaifa yalifanyika mkoani Simiyu, Wizara ya Afya Maendeleo ya Jamii, Jinsia,Wazee na Watoto ilieleza hali halisi ya tatizo la macho nchiini.

**HALI INAYOTAWALA**

Dk. Grace Maghembe ni Mkurugenzi wa Idara ya Tiba Wizara ya Afya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, anasema inakadiriwa kuwa Watanzania 600,000 hawaoni.

> "Asilimia 89 ya wenye upungufu wa kuona, wanaishi katika nchi za uchumi wa chini na wa kati, ikiwamo Tanzania.



Anasema, hali iliyopo ni muhimu mtu akafika kwanza hospitalini mara tu anapohisi matatizo ya macho na sio kukimbilia kutumia dawa, ama iwe rasmi au si rasmi.

"Watanzania 600,000 hawaoni na wenye matatizo ya kuona kwa kiwango cha kati na cha juu wanakadiriwa kuwa ni mara tatu ya watu wasioona, ambao ni takriban milioni 1.8, hivyo Tanzania ina watu milioni 24 wenye matatizo ya kuona," anasema Dk, Maghembe.

Anafafanua, kuwapo watu milioni 24 sawa na asilimia 2.5 ya Watanzania wote, wana ulemavu wa kutokuona ikijumuishwa na upungufu wa kuona.

"Upungufu huo wa kuona unarekebishika kwa miwani asilimia 45, mtoto wa jicho asilimia 28.8, shinikizo la jicho asilimia nane, kovu kwenye kioo cha mbele cha jicho na Trakoma asilimia tano," anasema Daktari Maghembe.

Anaendelea kwamba kuna athari ya ugonjwa kisukari kupatikana kwenye pazia la jicho kwa watu wazima, ambazo ni asilimia nne, matatizo ya kutokuona ututoni asilimia mbili na mengineyo asilimia 8.2.

**VIPI DUNIANI?**

Anasema, watu bilioni 1.1 duniani wana upungufu wa kuona vizuri na kuna wakati wangeweza kusoma, ila kuna sababu wamekosa miwani kusaidia.

"Pia, takribani watu milioni 253 duniani wanakadiriwa kuwa na upungufu wa kuona kwa namna moja ama nyingine na kati ya hawa, milioni 36 wana ulemavu wa kutokuona kabisa," anasema.

Dk. Maghembe anasema asilimia 89 ya wenye upungufu wa kuona, wanaishi katika nchi za uchumi wa chini na wa kati, ikiwamo Tanzania.

Pia, anafafanua asilimia 75 ya ulemavu utokanao na upungufu wa kuona wa kati na wa juu, unaepukika kwa asilimia 55 ya wenye upungufu wa kuona wa kati na wa juu ni wanawake.

Anaongeza kuwa, ulemvu utokanao na upungufu wa kuona umepungua hadi asilimia 2.7 kwa mwaka 2020, ikilinganishwa na asilimia 4.6 ya mwaka 1990, ikitajwa kuwa mafanikio ya azimio la Dira ya Haki ya Kuona ifikapo mwaka huu.

**ELIMU KWANZA**

Mkurugenzi Msaidizi wa Magonjwa Yasiyo ya Kiuambikiza, Dk. James Kiologwe, anasema mwaka huu, walijikita zaidi kuelimisha watu wajikinge kupoteza uoni wa macho.

"Tulijikita zaidi katika utoaji elimu na tumewafikia wadau ili kuhakikisha huduma za macho zinakuwa bora zaidi kwa kila mtu na watu 450 kati ya milioni moja wamepatiwa huduma za upasuaji wa macho lengo, likiwa ni kuhakikisha wanapona," anasema Dk. Kiologwe.

Rais wa Chama cha Madaktari wa Macho Tanzania Dk. Frank Sandi, anasema kuna baadhi ya hospitali hazina madaktari wa macho, hivyo ni muhimu kushirikiana na serikali na wadau kuhakikisha mikoa yote inapata huduma hizo za macho.

Bingwa wa Magonjwa ya Macho kutoka Hospitali ya Benjamin Mkapa jijini Dodoma, Dk. Jasinta Feksi, anasema, mfumo wa hewa na moshi una athari kwa afya ya macho, huku akibainisha miwani ya jua ina madhara kwa macho, ikiwamo kuota nyama.

Mdau wa Afya ya Macho, Nesia Mahenge wa Taasisi ya Christofeel Blinden Mission (CBM), anachagia kuwapo tatizo la upatikanaji takwimu za enye matatizo ya macho nchini.

AFYA

MKASA WA ALIYEDONDOKA GHOROFANI...

# Miaka 13 maisha yahamia hospitalini hajiwezi, vidonda, mke naye ayeyuka

- Waliomliwaza kulea mtoto watangulia
- Alia kutoweka aliyechangia kuanguka

**Mary Mosha,** MOSHI

"KWA sasa mimi sijui hatima ya maisha yangu. Natamani kuanza maisha mapya ya uraiani, lakini sina uwezo. Mke wangu alinikimbia nikiwa hospitalini mauti uti siwezi kujigeuza,' anaanza simulizi Paulo Matemu (45) mkazi wa Kijiji cha Kileo Kati, Kata ya Kirua Vunjo, wilayani Moshi, Mkoa Kilimanjaro

"Wazazi wangu na ndugu zangu waliokuwa na uwezo wa kunisaidia kupeleka mkono kinywani, matibabu, mazoezi na dawa wameshafariki. Aliniachia mtoto mdogo wa miaka sita

"Vitu tulivvyokuwa navyo aliviuza na vingine kupeleka kwa ndugu zake walio karibu, baada ya mimi kupata ajiali na kulazwa hospitali kwa mwaka moja tu. Simlaumu kwa kuwa naamini Mungu bado ana mipango na mimi," anasimulia katika utashi uliojaa malalamiko.



Paulo Matemu akiwa hospitalini. **PICHA: MARY MOSHA**

### KULIKONI KUANGUKA?

Matemu aliyepitia hospitali mbalimbali nchini kwa zaidi ya miaka 13, hivi sasa yuko katika hospitali ya Kilema, Moshi alikolazwa kwa miaka nane mfululizo, anajitambulisha kuwa mzaliwa wa sita katika familia ya watoto 10 ya Mzee Wilbard Matemu.

Alipata elimu ya msingi katika shule ya Msufini na baadaye sekondari ya Kisomachi, alikoshindwa kumaliza kutokana na kukwama ada alipokuwa kidato cha pili.

Baada ya muda, alijiunga na Chuo cha Ufundi Arusha alikopata mafunzo ya mwaka mmoja ya ufundi, iliyomuwezesha kuanza kufanya kazi ndogo za ujenzi kwanzia mwaka 1994.

"Niliendelea kufanya kazi zangu kwa ufanisi mkubwa na watu waliniamini na kunipa kazi zao, hadi mwaka 2007 nilipopatana na tajiri mmoja kusimamia ujenzi wa ghorofa katika maeneo ya Ilboru.

"Nilifanya kazi ile na kukamilika vyema, ingawa tajiri alianza kunizungusha na fedha na siku ya mwisho alinitaka nirudi baada ya wiki mbili na muda ulipotimia nilifika na alinitaka nifanye marekebisho eneo dogo la dirisha palipokuwa pamemeguka.

"Niliweka mbao ili iweze kunisaidia kufanya marekebisho hayo na bahati mbaya, mbao hiyo ilikuwa imepekechwa na kavu, ikavunjika na nikaanguka kutoka ghorofani mpaka chini," anasimulia.

Matemu anasema baada ya tukio hilo hakujua kilichoendelea mpaka siku ya tatu alipojikuta katika Hospitali ya Rufani Mkoa Arusha - Mount Meru, amepoteza hisia za kusikia chochote kuanzia kiunoni hadi miguuni.

"Nilipozinduka nilimkuta muuguzi, daktari, wazazi wangu, kaka zangu wawili na dada mmoja. Daktari alinipa pole na kuniambia nimepata shida kwenye uti wa mgongo.

"Machozi yalimtoka mama yangu na kisha akanishika mkono na kuniambia 'Mwanangu usiogope Mungu yupo utapona' na kisha akatoka nje,"anasimulia Matemu.

> **Nilipozinduka nilimkuta muuguzi, daktari, wazazi wangu, kaka zangu wawili na dada mmoja. Daktari alinipa pole na kuniambia nimepata shida kwenye uti wa mgongo.**

Anasema aliendelea kupata matibabu kwa miaka katika Hospitali ya Mount Meru, kisha alihamishiwa Arusha na baadaye Hospitali ya Rufani Mwananyamala, Dar es Salaam, huku familia ikiendekeza jitihada za kumhudumia.

### MKE ATOWEKA

"Mke wangu tuliyekuwa tumejaliwa mtoto moja, alikuja naye hospitali na kunitaka nibaki naye yeye anakwenda kutafuta pesa kwa ajili ya kuhudumia familia, kisha akaondoka simu zake hazikupatikana tena mpaka leo, baba yangu alipokuja hospitali nilimpa mwanangu wakamlee, "anasema huku machozi yakimtiririka na kuyafuta, analitaja kuwa tendo lililoishangaza familia yake.

"Niliendelea na matibabu kwa mwaka moja na nililazimika kuhamishiwa Hospitali ya Rufani KCMC kutokana na daktari bingwa wa mazoezi kustaafu. Nilipofika huko, huduma hazikuwa nzuri sana na familia yangu iliamua kunipeleka Mwananyamala Dar es Salaam," anaendelea.

Anasimulia mwaka 2012 alirejeshwa nyumbani kuendelea na matibabu ya vidonda, lakini huduma duni zilimfanya apelekwe tena katika Hospitali ya Kilema mwaka 2013, ingawa anasema hakupata nafuu kubwa ya vidonda, kwa kushindwa kujihudumia, haja zote kufanyika kitandani.

"Tulijaliwa mtoto mmoja... alikuja naye hospitalini siku alipokuja kunipa taarifa ya kuondoka kwake, ikiwa ni mwaka mmoja tu tangu nipate ajali hiyo, mtoto alikuwa na miaka sita tu.

"Kwa kuwa nilikuwa katika hali ya mauti siwezi kujigeuza, nililazimika kuwaomba wazazi wangu wakae na mwanangu, "anasema na mara baada ya kupata nafuu, alianza jitihada kumtafuta mkewe bila ya mafanikio, ingawa dada wa mke (shemeji) alidai ameshaolewa na mwanamume mwingine, kutoka mkoa tofauti.

Anasema, pia hajawahi kumshuhudia mhusika wa jengo alikokuwa anamhudumia, ingawa anakiri sura ya pili hawakuwa na mkataba rasmi wa kimaandishi.

"Tajiri yangu hakuwahi kuja kunitazama hospitali wala kunipa akiba yangu iliyobaki... nimeshindwa kupata haki zangu na naiomba serikali chini ya wizara husika kuhakikisha wanasimamia mafundi kuingia mkataba kabla ya kuanza kazi yoyote," anasema.

Matemu anasema mtoto aliyewakabidhi wazazi miaka mitano baadaye nao walifariki, hivyo amemuomba mtu tofauti kumsitiri mtoto huyo, katika mazingira si imara sana katika uchumi wa kila siku kimaisha.

"Mimi binafsi sijiwezi, nipo hapa hospitalini siwezi kufuatilia kama baba yake, kwani sijafanikiwa kumlea licha ya kuwa nilikuwa na ndoto za kumsomesha na kumlea katika misingi impendezayo Mungu, ili aje kuwa msaada kwa familia yangu na jamii inayomzunguka," anasema.

"Kwa sasa sijui maendeleo yake, lakini kwa ninavyoelezewa siridhishwi na ufaulu wake. Sina namna zaidi ya kumsisitiza asome kwa bidii," anasema,

### HOSPITALINI KILEMA

Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Kilema, Sista Dk Mayola Masawe, anasema hadi sasa Matemu hadaiwi chochote hospitalini hapo alikokuwa kwa miaka nane, ikijumuisha huduma za kulazwa, chakula na upasuaji.

"Niliingia hapa 2018 kama daktari, nilimkuta Paulo () Matemu) ana vidonda vingi, alikuwa akifanyiwa usafi kila siku, lakini hali yake ilionekana kuwa mbaya hadi Julai 2019 tuliwasiliana na madaktari bingwa wa Hospitali ya Rufani KCMC.

"Walifika hapa Kilema na tukajadili namna ya kumsaidia, walishauri afanyiwe upasuaji kwa jili ya kugeuza mfumo wa haja kubwa kutokea ubavuni, badala ya sehemu husika ili kuruhusu vidonda kupona.

"Vidonda vyote vilivyomsumbua kwa muda mrefu, vina nafuu kubwa na kama haikutokea tatizo lingine baada ya miezi minne tutamruhusu kuelekea nyumbani kwa ajili ya kwenda kuanza upya." anaeleza daktari huyo.

"Kwa miaka nane ameishi hapa Kilema, hakuna wa kumsaidia na ombi lake ni kupata nyumba yenye miundombinu rafiki kwa ajili ya ulemavu wake, ingawa anaweza kufanya shughuli zake mwenyewe.

"Pia, italazimika kupata fedha za kujikimu kununua mipira ya kubalilisha angalau kwa apate laki moja kwa mwezi,"anaeleza.

Rai ya Matemu, iwapo atapata msamaria wa kumsaidia fedha kwa ajili ya mahitaji muhimu, makazi na nyenzo ya usafiri, pamoja na mtaji wa kujikimu kimaisha itakuwa msaada kwake kwa maisha yajayo.

***Mgonjwa Paulo Matemu anapatikana kwa simu: 0710858334/0747138191 na mwandishi 0621066808; Usikose mkasa mwingine Alhamisi ijayo.***

AFYA

# Kuugua Trump na alivyyopona haraka, darasa la tiba wagonjwa corona wazee



Rais Donald Trump, alipoagana na daktari wake hospitalini. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

**Na Michael Eneza**

PILIKA za siasa za Marekani zimefikia kileleni mwishi wa wiki iliyopita, Joe Biden, kutoka chama cha Democrat, amekichukua kiti cha urais wa Marekani.

Sehemu ya maudhui yake, ni sera za kukabili maradhi ya corona aliyeangaliwa sana hadi 'majuzi' ni sera, matendo na misimamo ya anayeondoka Donald Trump, ambaye alikutwa na corona

Kidokezo cha aliyewahi kudokeza kupania kusambaratisha 'corona' juzi aliweka mambo hadharani kwamba ataanza kwa kuunda bodi ya ushauri kuhusu namna kupamba na maradhi hayo.

Lakini kwa kurejea nyuma, utafiti kuhusu namna chanjo ya corona, au tiba zinazoaminika, unaelekezwa ulipata nguzo nzuri, kutokana na kuugua kwa muda mfupi Rais Donald Trump wa Marekani, aliyelazwa katika hospitali ya kijeshi iliyoko jirani na Ikulu, akatoka siku ya tatu.

Ilikuwa mazingira tofauti na jinsi alivyougua miezi michache iliyopita, Waziri Mkuu wa Uingereza, Boris Johnson, aliyefikishwa chumba cha wagonjwa wa uangalizi wa karibu (ICU) na alipotoka hospitalini Trump hakufuata taratibu za kujifungia kuogopa kuambukizwa au kuambukiza, alirudi kwenye kampeni za uchaguzi kama nyati aliyejeruhiwa.

Hapo ndipo kuna jambo alilosema Trump baada ya kuonekana hana virusi vya corona na hivyo akapata kibali cha kufanya kazi zake kama watu wengine, huku akijisifu kuwa 'sasa haambukizwi tena corona' kwani kuugua kwake na kutibiwa ameshajenga kinga.

Hilo nalo halina uhakika, kwani wataalamu wanasema kinga zinazotokana na kupona corona hazidumu ila kwa miezi michache na inabidi bado ufanyike utafiti wa kina, au ukamilishwe vyema zaidi, kama ni kwa kasi gani na watu wa aina gani kinga hizo hupotea haraka zaidi. Ila ugonjwa wa Trump umekuwa kielelezo maalum cha ugonjwa, kwa umri wake, mazingira ya kiafya, kupona kwake na dawa zilizotumika, kwani chanjo zilizojaribiwa zimegota.

> **Tofauti kati ya utafiti tiba za chanjo au dawa nyingine kati ya nchi za Magharibi ikiwamo Marekani na China au Russia, ni kwamba nchi za Magharibi zina taratibu mgumu kwa ugunduzi wa dawa au chanjo kuthibitishwa.**



Rais Donald Trump, akiwa na barakoa hospitalini.

Tukio la Trump kuugua corona ni kama jaribio la kisayansi la uwezekano wa kupona, tena kwa haraka, kwa mtu mwenye umri wake (miaka 74), mwenye kila dalili za uzito wa ziada na kwa maana hiyo, kuwa na chembe za msukumo ziada wa damu au kwa lugha maarufu 'BP'na kadhalika.

Baadhi ya maelezo kuhusu tiba yake yanafafanua kuwa, alipatiwa aina yadawa inayotumika kwa watu mahututi, hoja inayobeba maana kuwa alipewa dozi kali kuliko ambayo ingepasa, kwa vile iliwezesha kupona haraka na kurudi tena kwa nguvu katika kipindi ambacho hawezi kufanya kazi rahisi ofisini, si labda ndiyo itumike zaidi?

Baada ya kupona, Trump alisema inawezekana kabisa kuugua kwake kulikuwa alichokiita kwa kizungu 'a blessing in disguise' (baraka iliyojificha) kwa maana mbili muhimu.

Kwa upande wake ni kama imempa nguvu mpya kutokana na kuwa na kinga na akawa anasisitiza kwa mashabiki wake kuwa "mimi nina kinga, Biden (mgombea pinzani) hana."

Biden anamzidi Trump kwa umri miaka mitatu, lakini bado kuna suala la utafiti kama akiugua akatibiwa matokeo yake yatakuwa kama ya Trump au inategemea kama ana hitilafu nyingine. Ila ukweli yuko 'fiti' hajikongoji katu.

Nje ya maana hiyo binafsi, maana pana zaidi ya 'baraka iliyojificha' ya kuugua Trump na kupona virusi vya corona ni uhakika wa masuala kadhaa ambayo utafiti ungechukua muda mrefu kukubaliana, hasa kwa vile corona imekuwa hatari zaidi na kusababisha vifo kwa haraka kwa watu wenye umri wa zaidi ya miaka 65.

Trump alikuwa kielelezo maalum, kwani ana umri karibu miaka zaidi ya kiwango hicho ambacho madaktari wanaona ni cha hatari. Ni watu wanaohitajiwa kujizuia wenyewe wasitoke sana kwenda mbali, kwani wakiambukizwa kupona kwao ni mtihani.

Kupona Johnson wa Uingereza ilikuwa tabu, ikiambatana na woga wa siku kadhaa kuwa angeweza kupoteza maisha wakati wowote; hiyo haikutokea wakati Trump akiugua.

Sasa inajulikana kuwa kwa watu wa umri wa Trump,, dawa aliyotumia (au mchanganyiko uliotumika) hauna haja ya kungojewa hadi mtu afikie mahututi ndiyo itumike ila ingeanza hiyo matokeo yangeweza kuwa mazuri zaidi, kama ya Trump.

Ina maana kuwa licha ya 'kusulubiwa' katika kampeni ya uchaguzi wa rais nchini humo, kuugua kwa Trump ilikuwa kama kuyafakinisha anayozungumza, kwani kufikishwa hospitali na kukaa siku tatu hakukuleta woga maalum kuhusu uvaaji wa barakoa.

Licha ya maofisa kadhaa wa Ikulu nao kupata corona kama yeye, walijitahidi kuhusu kuacha nafasi (social distancing) wakati wa mikutano yao na hata hivyo kwa tabu na hadhara zisizojaa watu kuendelea Ikulu.

**SOMO KUU LILIPO**

Kuugua Trump na kisha akapona kwa haraka, kumetoa mwanga kuhusu matumizi ya dawa zenye uwezo kutibu haraka virusi vya corona, wakati ambao utafiti wa chanjo hadi sasa unasuasua.

Majaribio mawili yalikwama kuendelea, kutokana na mtu aliyeko kwenye kundi (linalojumuisha maelfu ya watu) katika majaribio ngazi ya tatu kuugua ghafla, kwa chanjo ya AstraZeneca na Chuo Kikuu cha Oxford, halafu chanjo iliyofanyiwa utafiti ya Johnson &Johnson.

Nchi ambazo hadi sasa zimepitisha chanjo na zinatumika ni Russia, chanjo inayoitwa Sputnik 5 iliyoetengenezwa jeshini; China haijapiga kelele kuhusu chanjo yake ya Sinocovax (au kwa kitaalamu Ad5-nCoV) iliyotengenezwa na kampuni ya CanSino Biologics, inayoshirikiana na tawi la utafiti wa dawa na mahitaji tofauti ya jeshi la China.

Tofauti kati ya utafiti tiba za chanjo au dawa nyingine kati ya nchi za Magharibi ikiwamo Marekani na China au Russia, ni kwamba nchi za Magharibi zina taratibu mgumu kwa ugunduzi wa dawa au chanjo kuthibitishwa.

Nchi za 'mashariki' zinapofikia dawa ya kumtibu mtu mmoja au kundi la watu bila udhaifu wowote kujitokeza, mamlaka za nchi zina uwezo wa kuamua kama ianze kutumika, kwa mfano Russia ilianza kutumia chanjo ya Sputnik 5 jeshini.

Hata madaktari wa Trump, walisema walitumia dawa hiyo kwa majaribio, ambayo ina maana hawakuwa na dawa bora zaidi, ila kwa matokeo yake, unaweza kusema kuwa wako salama, kwani huwezi kupata mgonjwa wa umri wa Trump, atumie dawa atoke hospitalini akiwa na nguvu na ari ya kuchapa kazi kama Trump. Ni uthibitisho kuwa inafaa kutumika.





# EWURA yawafunda wenye ualbino

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MAMLAKA ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), imewaomba watu wenye ualbino kuwa mabalozi wa kutoa elimu kwa wenzao, ili kusaidia kujua wajibu wa watoa huduma na watumiaji.

Akizungumza jana kwenye semina ya uelimishaji kwa watu wenye ulemavu wa ngozi iliyoandaliwa na Mamlaka hiyo, Meneja wa EWURA Kanda ya Kati, Norbert Kanyoza, alisema kundi hilo ni muhimu kusaidia kutoa elimu kwa wengine ili kutambua haki zao za msingi kama watumiaji. "Kundi hili liwe balozi wa huduma zetu kwa umma uliobaki nje, rai yetu mtakapoelewa EWURA ni nani na anafanya nini mtusaidie kueneza elimu hii kwa wengine ambao hawajapata bahati ya kuhudhuria semina hii," alisema.

"Tunatoa elimu kwa kundi hili juu ya majukumu yetu matarajio ni kama walivyosema wanataka kujua EWURA kwa kina na tumewaeleza tupo wapi tunafanya nini masuala ya leseni na kuadhibu mtoaji wa huduma anapokiuka matakwa ya leseni."

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya kuongeza uelewa kwa jamii juu ya watu wenye ualbino (AAF), Selemani Magoma, alisema semina hiyo inalenga kuhamasisha ushiriki wa kundi hilo katika shughuli mbalimbali za maendeleo nchini.

"Tunashukuru sana EWURA kwa kuwatambua watu wenye ualbino kama wadau muhimu wa masuala ya kimaendeleo na kuona umuhimu wa kuwashirikisha katika kuwapa elimu kuhusu kazi na majukumu mbalimbali ya EWURA," alisema.

Alisema elimu hiyo ni muhimu kwa kuwa ni watumiaji wa huduma zinazotolewa na mamlaka hiyo.

"Semina ya leo ni mwanga tumejua majukumu ya mamlaka hii tukitegemea watakuwa mabalozi wa kazi zinazofanywa na EWURA na watashiriki kikamilifu, na tunashukuru serikali kupitia mamlaka hii kwa kuona hawa ni wadau muhimu wa maendeleo," alisema.

Mwenyekiti wa watu wenye ualbino Dodoma, Ludovick Julius, alishukuru mamlaka hiyo kwa kutoa elimu hiyo ambayo alisema italeta manufaa kwao na namna ya kutoa mapendekezo yao kama kuna tatizo kwa watoa huduma.



Baadhi ya wageni kutoka maeneo mbalimbali nchini wakiingia kwenye viwanja vya Bunge, jijini Dodoma jana, kwa ajili ya kushuhudia kuapishwa kwa wabunge wao. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Zaidi ya mbwa 500 wanaofugwa wapewa chanjo

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

HALMASHAURI ya Jiji la Dodoma imetoa chanjo ya mifugo kwa mbwa 502, wanaofugwa majumbani ili kukabiliana na magonjwa mbalimbali hususani tatizo la kichaa cha mbwa.

Mkuu wa Idara ya Mifugo na Uvuvi wa Halmashauri ya Jiji la Dodoma, Gration Mwesiga, alibainisha hayo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu operesheni ya utoaji chanjo kwa wanyama inayotekelezwa na wataalamu wa mifugo.

Mwesiga, alisema lengo ni kufikia mbwa wote wanaofugwa katika jamii ili kuepuka kuleta madhara kwa watu, hususani kichaa cha mbwa wanapowangata binadamu.

Alisema kuwa, pamoja na watu wengi kufuga mbwa, lakini hawawapeleki katika chanjo, jambo ambalo halikubaliki kitaalamu.

"Tumejipanga kuhakikisha tunatoa chanjo kwa mbwa wote hapa jijini, tunahitaji kuona mbwa wanaofugwa wanakuwa katika hali ya usalama ili wasilete matatizo kwa jamii," alisema Mwesiga.

Alisisitiza jamii kuhakikisha wanapeleka mifugo yao kupata chanjo pale wanaposikia kuna utoaji huduma hiyo, zoezi linalotekelezwa na watalaamu wa mifugo, katika maeneo yao.

Alisema, hakuna sababu ya wao kufuga mifugo, bila kufuata taratibu za kiafya kwa wanyama ambayo inawasaidia kuwa katika hali ya usalama.

Pia, alisema bado wataendelea na operesheni ya kuua mbwa wanaozurura mitaani ili kuepusha kuleta madhara ya kichaa cha mbwa.

Alisema kumekuwa na tabia ya jamii kufuga mbwa na kuwaachia wakizurura ovyo kitendo kisichokubalika na idara ya mifugo inaendelea na operesheni hiyo.

"Bado tunaendelea na zoezi la kuua mbwa wazururaji lengo ni kuepusha kuwasababishia binadamu kichaa cha mbwa," alisema Mwesiga.

Aidha, alisema operesheni hiyo imefanyika katika mitaa mbalimbali jijini Dodoma na kudai kuwa wataendelea kuwasaka mbwa hao na kuwatokomeza kabisa.

Aliwataka wananchi kutoa taarifa wanapoona kuna mbwa wanazurura ili wasiendelee kuleta madhara.

Kitaalamu alisema, mbwa mzururaji hupata kichaa, kutokana na kukosa matunzo au kuumwa na wanyama wengine kama paka na fisi ambao humsababishia kichaa.

## RC aingilia kati mgogoro ardhi wananchi/kanisa

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MKUU wa Mkoa wa Dodoma, Dk. Binilith Mahenge, ameiagiza Mamlaka ya Mipango Miji ya Jiji la Dodoma na kamati maalumu iliyoundwa kuchunguza mgogoro wa ardhi kati ya wananchi wa kijiji cha Chigongwe na Kanisa la TAG Jimbo la Dodoma, kuleta hati zote zinazoonyesha umiliki wa ardhi hiyo.

Dk. Mahenge alitoa agizo hilo jijini hapa alipotembelea eneo lenye mgogoro na kupokea ripoti ya kamati hiyo na kutoa siku 14, kwa mamlaka hiyo na kamati kuleta hati zinazoonyesha nani mmliki halali wa eneo hilo.

"Nawapa siku 14, nataka mlete hizo nyaraka mimi nizione na nyingine ziende kwa Mkuu wa Wilaya ili tuthibitishe, je, ni kweli watu waliuziwa maeneo hayo wanamiliki ardhi hizo kihalali," alisema Dk. Mahenge.

Pia, aliagiza mamlaka hiyo kwenda kupitia eneo hilo na kupima maeneo yote ambayo hayajapimwa na kumilikishwa.

"Mipango miji mpitie eneo hili lote mkitoa maeneo ya milima na maeneo yaliyomilikishwa wananchi kihalali linalobaki wapewe wawekezaji hawa na kumilikishwa bila gharama yoyote isipokuwa zilizopo kisheria," alisema.

Aliwataka wawekezaji hao ambao ni Kanisa la TAG kukubali kupokea eneo hilo litakalobaki, huku akikiri kuna udhaifu uliofanywa na iliyokuwa Mamlaka ya Ustawishaji Makao Makuu (CDA).

Mwenyekiti wa Kamati Maalumu iliyoundwa kuchunguza mgogoro huo, Mhandisi Happiness Mgalula, alisema wamepitia maeneo hayo na kukutana na pande zote mbili.

Alisema kuwa kuna nyaraka zinaonyesha Kanisa la TAG, walipewa eneo hilo na uongozi wa Kijiji cha Chigongwe, lakini kuna baadhi ya nyaraka hazikupatikana.

"Tumepitia maeneo yote na kubaini CDA, iliomba andiko la mradi kwa kanisa, lakini hakuna nyaraka zinazoonyesha kuwa CDA ilijibiwa na kanisa, japo kuwa kanisa linadai lina nakala ya barua ya andiko walilotuma CDA," alisema.

Kaimu Ofisa Mipango Miji Jiji la Dodoma, Emelye Chaula, alisema kuna nyaraka zinaonyesha kanisa lilipewa eneo lenye ekari 200 na kijiji, lakini baada ya CDA kupima walikuta ekari 560.

"Lakini Jiji kupitia wataalamu wake waligundua kuwa eneo hilo lina ekari 635.7 wakaanza kujiridhisha kama kuna upimaji wowote uliwahi kufanyika na kubaini tangu mwaka 2013 kipindi cha CDA kuna taasisi nyingine na watu binafsi walipimiwa viwanja ndani ya viwanja hivyo vya kanisa," alifafanua.

Askofu wa kanisa hilo, Jimbo la Dodoma, Stephen Mahinyira, alisema eneo hilo walipewa na uongozi wa kijiji cha Chigongwe mwaka 2009 na baada ya hapo wakaanza kufuatilia nyaraka za umiliki kihalali CDA, lakini mpaka sasa hawajafanikiwa.





# Wakulima kahawa waingiwa na hofu

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

BAADHI ya wakulima wa kahawa mkoani Mbeya, wameanza kupata wasiwasi wa kushuka kwa soko la zao hilo kutokana na tishio la ugonjwa wa corona kutokana na wanunuzi wengi kutoka nje ya nchi.

Wakizungumza na Nipashe kwa nyakati tofauti juzi, wakulima hao katika bonde la Utengule katika Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mbalizi, walisema wanapata hofu hiyo kutokana na mataifa mengi kusitisha biashara.

Mmoja wa wakulima hao, Joseph Mwashitete, alisema kahawa ni tofauti ni mazao ya chakula kwa kuwa soko lake la ndani ni dogo kuliko la nje na kwamba wanazalisha zao hilo kutokana na hamasa wanayoipata kutokana na soko la nje.

Alisema baadhi ya kampuni kutoka nje ya nchi zimekuwa zikiwakopesha hata pembejeo kwa ajili ya zao hilo, lakini kwa sasa kuna hatari ya mikopo hiyo kusitishwa na uzalishaji kuporomoka.

"Mazao ya chakula hata tusipouza huwa tunakula wenyewe, lakini kahawa hata gunia moja mimi na familia yangu hatuwezi kutumia tukamaliza kwa mwaka. Sasa mataifa tunayoyategemea ndiyo yanayokabiliwa kwa kiasi kikubwa na tatizo la corona," alisema Mwashitete.

Alisema wasiwasi mkubwa wanaupata kutokana na serikali za mataifa mengi kuanza kusitisha mwingiliano wa watu kutoka mataifa mbalimbali kusitisha biashara ya ununuzi wa zao hilo, ili kukabiliana na corona.

Naye Nathan Mbwaga, ambaye ni mkulima wa kahawa katika Kijiji cha Itimba, alisema sasa msimu wa kahawa kuanza kuchumwa unakaribia, lakini mpaka sasa kampuni yaliyoanza kuonyesha nia ya kwenda kununua ni machache.

Aliiomba serikali kuendelea kutoa elimu kwa wananchi wa kada zote, ili ugonjwa huo usiendelee kuenea kwa maelezo kuwa ukisambaa sana hata soko la ndani la kahawa litakuwa dogo.

Alisema uzalishaji wa zao hilo umekuwa ukiongezeka kila mwaka kutokana na mahitaji ya soko la dunia na kwamba kwa sasa wana wasiwasi kuwa hata kiwango cha uzalishaji kitashuka kutokana na kuporomoka kwa soko.

# Viongozi wakumbushwa kufuata taratibu kuhusu ugawaji ardhi

**Na Grace Mwakalinga,** MBARALI

VIONGOZI wa vijiji vyote vinavyounda Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali mkoani Mbeya, wameshauriwa kufuata taratibu za kisheria katika kugawa maeneo kwa wawekezaji.

Miongoni mwa taratibu hizo ni kuwashirikisha wananchi badala ya kujiamulia ili kuepuka migogoro kati ya wananchi na wawekezaji.

Ushauri huo ulitolewa jana na Ofisa Mipango Miji katika Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Enock Kyando, alipokuwa akizungumza na Nipashe kuhusu hatua mbalimbali walizozichukua katika kukabiliana na migogoro ya ardhi wilayani Mbarali.

Kando ambaye ni Mjumbe wa Kamati Maalumu ya Uelimishaji Wananchi kuhusu umuhimu wa uhifadhi na ujirani mwema, alisema mkutano mkuu wa kijiji ndio wenye mamlaka ya kugawa ardhi ya kijiji.

Alisema kazi ya viongozi wa vijiji hasa Ofisa Mtendaji na Mwenyekiti ni kupokea maombi ya wanaotaka kupewa ardhi na kuitisha mkutano wa vijiji ili wananchi wajadili na kuridhia au kutoridhia kugawa ardhi kulingana na uhitaji.

"Msimamizi mkuu wa ardhi ya kijiji ni wanakijiji wenyewe na ndio wanaotakiwa kuamua kumpa mtu mwingine ardhi yao kwa ajili ya matumizi ambayo wataona inafaa. Kiongozi ukifanya maamuzi (uamuzi) mwenyewe unasababisha migogoro," alisema Kyando. Alisema kwa mujibu wa Sheria ya Ardhi, kijiji kinaruhusiwa kugawa ardhi isiyozidi hekta 50 kwa mtu mwingine na kwamba ikizidi ukubwa huo, kuna mamlaka zingine ambazo zinahusika na hivyo mhitaji wa ardhi hiyo atatakiwa kuziona.

Kuhusu mpango wa matumizi bora ya ardhi, Kando alisema kila kijiji kinatakiwa kuwa na matumizi bora ya ardhi kwa maelezo kuwa utaratibu huo unasaidia kuondoa migogoro ya ardhi kwa kuepusha mwingiliano wa shughuli za kibinadamu.

Ofisa Ardhi wa Wilaya ya Mbarali, George Mwaijobelo, alisema wilaya hiyo imekuwa ikikabiliwa na migogoro mingi ya ardhi kutokana na vijiji vingi kutokuwa na mipango ya matumizi bora ya ardhi.

Alisema kutokana na elimu ambayo kamati yao inaitoa kwa wananchi baadhi ya vijiji vimeanza kuwa na uelewa na kwamba vijiji hivyo vimeanza kupanga matumizi bora ya ardhi.

"Ardhi yetu haiongezeki, lakini binadamu tunaongezeka na mifugo yetu inaongezeka. Kwa hiyo ni lazima tuwe na matumizi bora ya ardhi kulingana na shughuli zetu za kiuchumi na kijamii," alisema Mwaijobelo.

Alisema baadhi ya maeneo yanatakiwa kutengwa kwa ajili ya kilimo, makazi, kuchungia mifugo na shughuli zingine za kijamii ikiwamo maeneo ya viwanda na taasisi za serikali.



Mkuu wa Wilaya ya Mbarali, mkoani Mbeya, Reuben Mfune (kushoto), akikabidhi simujanja kwa mmoja wa maofisa uandikishaji wa Mfuko wa Bima ya Afya iliyoboreshwa (CHF), zilizotolewa na halmashauri ya wilaya hiyo, jana ili kurahisisha utendaji kazi hususani vijijini. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# Waandikishaji CHF wapewa vitendea kazi

**Na Grace Mwakalinga,** MBARALI

MKUU wa Wilaya ya Mbarali mkoani Mbeya, Reuben Mfune, amekabidhi simu janja 50 kwa maofisa waandikishaji wa Mfuko wa Afya ya Jamii (CHF) iliyoboreshwa ili kurahisisha kazi ya kuwafikia wananchi walioko pembezoni.

Mfune alikabidhi simu hizo juzi, katika ofisi za wilaya hiyo, huku akisema simu hizo zitasaidia maofisa kufanya mawasiliano kwa karibu na wanufaika wa mfuko huo na kuongeza kuwa lengo ni kuwafikia wananchi wengi zaidi katika uandikishaji.

Alisema Sh. milioni 8.5 zimetumika kununua simu hizo ili kuongeza ufanisi katika uandikishaji kupitia CHF.

"Simu hizi zitaongeza kasi kuandikisha kaya nyingi zaidi ikiwa ni pamoja na kuhuisha kaya zilizoandikishwa kipindi cha nyuma. Mhakikishe mnaandikisha angalau kaya 20 kwa mwezi," alisema Mfune.

Aliwaomba maofisa kuhakikisha wanafikia lengo la kuandikisha kaya 20,000 hadi kufikia Desemba, mwaka huu, na kwamba kazi hiyo itakuwa endelevu.

Mratibu wa CHF, Stephen Bitta, alisema Wilaya ya Mbarali ilianza utekelezaji wa mfuko huo Mei, 2019 na hadi kufikia sasa imeandikisha kaya 1,614 sawa asilimia 2.3 ya lengo la kaya 69,667 au sawa na asilimia 8.07 ya lengo la mwaka la kaya 20,000.

Aliongeza kuwa uandikishaji wa wanachama wa CHF umetofautiana kati ya kitongoji, kijiji na kata moja na nyingine kutokana na sababu mbalimbali kama vile mwitikio wa jamii, uwezo wa waandikishaji walioteuliwa, vitendea kazi na mwingiliano wa maambukizi ya ugonjwa wa corona.

Wakizungumza kwa niaba ya wenzao kwenye ugawaji wa vitendea kazi hivyo, maofisa waandikishaji wameushuruku uongozi wa wilaya kwa kuwapatia zana hizo ambazo kwa sasa zitawaongezea ari ya kufanya kazi kwa bidii.





# Makamu wa Pili awaonya watumishi kujipendelea safari

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdallah, amewataka viongozi na watumishi wa umma wajitambue na kujitathmini katika utekelezaji wa majukumu yao waliyopewa ili kiu ya kuwatumikia wananchi ifanikiwe vyema.

Alisema baadhi ya viongozi na watendaji watakaojihisisi kwamba hawaendani na kasi ya serikali iliyoanza kazi baada ya kumalizika kwa uchaguzi mkuu, ni vyema wakaondoka kwa heshima.

Alitoa kauli hiyo juzi, baada ya kupokewa kwenye ofisi yake mpya wakati akizungumza na viongozi wa idara na taasisi zilizo chini ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Vuga mjini hapa.

Alisema haipendezi kuona baadhi ya viongozi wa taasisi na wakuu wa vitengo wanajifikiria maslahi yao binafsi hasa fursa za masomo na safari za nje ya Zanzibar zinazoambatana na posho bila ya kujali haki za watendaji wao wa ngazi ya chini.

"Haipendezi na haitawezekana kuona viongozi waandamizi na wakuu wa taasisi wanajipatia posho ya safari na washindwe kuwapatia haki zao wafanyakazi wao wa ngazi ya chini," alisema Hemed.

Alisema akiwa mtendaji mkuu wa shughuli za serikali hatakuwa tayari kumbeba kiongozi au mtumishi yeyote aliyepewa dhamana na akashindwa kuitekeleza katika eneo lake la kazi.

Alionya akimgundua kiongozi anayetumia vibaya rasilimali za umma aelewe atakwenda na maji kwa vile hatasita kumchukulia hatua za kinidhamu mara moja kutokana na tabia hiyo mbaya isiyokubalika katika utumishi wa umma.

Aliwataka watendaji hao wa utumishi wa umma wajisafishe kwa vile wao ndio wanaosimamia utendaji wa serikali na kuacha malalamiko yasiyo na msingi na pale vinapojitokeza kikwazo katika uwajibikaji wao taratibu ziko wazi za kuwasilisha changamoto zao zinazowakabili katika ngazi ya juu.

Aliwataka viongozi hao wastaafu waendelee kuacha milango wazi kwa viongozi wapya, ili pale watakapohitaji mawazo na busara zao katika uwajibikaji wa utumishi wa umma kuitumia fursa hiyo adhimu.

Akimkabidhi ofisi pamoja na nyenzo za kazi mtendaji mkuu huyo mpya wa shughuli za serikali, Makamu wa Pili wa Rais mstaafu Balozi Seif Ali Iddi, alisema uteuzi wa Rais wa Zanzibar kumpa dhamana Hemed unatokana na ujemedari wake katika kusimamia maslahi ya wananchi.

Balozi Iddi, alisema kwa umahiri wake hana shaka na jukumu alilokabidhiwa na kuwaomba viongozi na watendaji wa ofisi hiyo waendelee kumpa ushirikiano kama aliyopewa yeye wakati wa utumishi wake.



Mwakilishi wa Jimbo la Bumbwini kupitia CCM, Mtumwa Peya, akila kiapo mbele ya Spika wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar, Zuberi Ali Maulid, jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Wasiojulikana wadaiwa kutia kinyesi kisimani

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WATU wasiojulikana wametia kinyesi katika kisima cha maji kinachotumiwa na wananchi wa shehia ya Kinuni, Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja.

Wananchi wa shehia hiyo wameiomba serikali na viongozi wa jimbo kuwawekea mazingira mazuri ya miundombinu ya maji katika eneo lao, ili kuepusha kutiwa vinyesi na watu ambao hawana maslahi mema na taifa.

Wakizungumza juzi na waandishi wa habari wananchi hao walisema kitendo kilichofanywa na baadhi ya watu katika eneo hilo hakileti taswira nzuri na maji hayo hutumiwa na watu wote bila kujali itikadi za kisiasa.

Haji Rajab Haji, balozi wa shehia ya Kinuni alisema tukio hilo lilitokea Novemba 8, wakati alipopewa taarifa na mtoto wake kwamba kisima kimetiwa kinyesi cha mtu. Pia, alisema hiyo ni mara ya tatu kisima hicho kutiwa kinyesi hali inayosababisha usumbufu kwa wananchi wa eneo hilo, kukosa miundombinu hiyo ambayo wanaitegemea kwa shughuli mbalimbali za kijamii.

Naye Zainab Issa, mkazi wa shehia hiyo, alisema kitendo cha kutiwa kinyesi katika kisima hicho kimewaathiri kwa kuwa kisima hicho wanakitegemea kupata maji ya kunywa, kupikia, kufulia na shughuli nyingine za kijamii.

Aliwaomba viongozi kuwajengea kisima ambacho kitawekewa miundombinu mizuri, ili kuepusha kufanyiwa hujuma hizo mara kwa mara.

Aliiomba serikali kuwekewa miundombinu ya mifereji (bomba) katika kisima hicho ambayo itakuwa suluhisho ya kuona maji hayo kuharibiwa mara kwa mara na watu ambao hawana dhamila njema na taifa lao.

Kwa upande wake mwakilishi wa jimbo hilo, Ali Suleiman Ameir, aliliomba Jeshi la Polisi kufanya uchunguzi wa tukio hilo ambalo litatahadharisha usalama wa afya za wananchi wa maeneo hayo.

Mwakilishi huyo aliwaomba wananchi kuendelea kupendana na kudumisha ulinzi na usalama ili maisha yao yaendelee kuwa mazuri.

Aliwaahidi wananchi hao kwa kushirikiana na viongozi wengine wa jimbo na serikali kukifanyia marekebisho kisima hicho ili wananchi wapate huduma hiyo kama kawaida.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mjini Magharibi, Awadh Juma Haji, alisema bado hajapokea taarifa za tukio hilo na kuwaomba wananchi kuliripoti ili kuhakikisha waliofanya tukio hilo wanachukuliwa hatua zinazostahiki.

Aliwaomba wananchi kulinda usalama katika maeneo yao, ili kuepusha miundombinu muhimu kama hiyo isiweze kuharibiwa.

## Ajira za watoto zinavyowanyima haki yao kielimu

**Na Mwandishi Wetu**

WADAU kisiwani Pemba, wameeleza kuwa kujiingiza katika ajira kwa watoto ni moja kati ya jambo linalowanyima fursa na haki zao za msingi za kupata elimu.

Walisema suala la msingi kwa watoto ni elimu na kuwataka wazazi na walezi wasibweteke na kipato cha wanachopata watoto hao badala yake wawazuie kufanya kazi hizo kwa kuwa zinawarudisha nyuma katika malengo ya maisha yao.

Wadau hao walisema wapo baadhi ya wazazi husingizia suala la umaskini kuwa ni chanzo kikubwa cha kuwaruhusu watoto wao kufanya kazi hizo, jambo ambalo sio sahihi.

Walisema hayo, kwa nyakati tofauti wakati walipokuwa wakizungumza juzi na waandishi wa habari kwa lengo la kukomesha vitendo hivyo, ambavyo vinawaathiri watoto hao.

Miongoni mwa wadau hao ni Mwanaharakati Hamad Khatib Hamad, alisema sababu kubwa inayochangia kuongezeka kwa ajira za watoto ni wazazi wenyewe pale wanapopelekewa pesa na watoto wao wakijua wamejishirikisha na ajira bila ya kuwakemea.

Alieleza ni jukumu la wazazi kuwafuatilia watoto wao katika masuala ya elimu na kujuwa kama watoto hao wanakwenda shule kwa wakati unaotakiwa, jambo ambalo litawaweka katika hali ya kujali elimu yao.

"Ajira za watoto zimekuwa ni tatizo katika maeneo mengi, lakini wazazi wasikubali wanapopelekewa kiwango cha fedha kutoka kwa watoto wao hata kama wamefanya kazi wakemee, ili watoto wapate elimu," alisema.

Khadija Saleh Mohamed, kutoka Mizingani mkoani Pemba, alisema ajira za watoto zinawafanya watoto wasifikie malengo yao kutokana na kuingiwa na tamaa wanapowaona wenzao wanapata pesa kwa kufanya kazi ikiwamo kugonga kokoto, kubeba mizigo na kupaa samaki.

Alisema wakati umefika wa kupinga ajira za watoto na zifanyiwe kila hatua, ili ziondoke kwa vile watoto wanaojishirikisha na ajira hizo hukata masomo yao shuleni na madrasa.

Akizungumzia sheria ya watoto inavyokataza ajira hizo, mwanaharakati kutoka mkoani, Nassor Hakim Haji, alisema, kwa mujibu wa Sheria ya Ajira Namba 11 ya mwaka 2015, imepiga marufuku ajira za watoto.

Alisema sheria hiyo imepinga vikali kuwatumikisha watoto katika ajira mbalimbali na kusisitiza kuwa endapo mtu atamtumikisha mtoto sheria imeweka adhabu ya faini ya Sh. 500,000 au kifungo kisichopungua miezi sita.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## VIWANJA NA MASHAMBA

**NYUMBA INAUZWA IKO KAHAMA** MAJENGO VYUMBA VITATU INA MAJI NA UMEME, PLOT No 759, BLOCK "E", KIWANJA NI MEDIUM SIZE. MAWASILIANO ZAIDI; 0759359933/0713553819

**NIPASHE NI JIBU LAKO**
**NJOO UTANGAZE NASI**
**KWA BEI NAFUU SANA**
Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0782253676

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**EFFCO (PTY) LTD**
Inatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya DAIWO yenye namba za usajili **T 263 BEV** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilicho karibu.
Taarifa ya polisi
**CONTROL NO. 9910819533050**

## TANGAZO
## KUPOTEA KWA CHETI



**ROSEMARY MAINRAD MWALONGO**
Amepotelewa na cheti cha kidato cha **NNE** alichomaliza ktk shule ya secondari **BUKUMBI GIRLS** mwaka 2015,chenye Index **no: S0235/0113/2015.** Yeyote atakaeiona anaombwa atoe taarifa kituo chochote Cha polisi

**RB Namba: MOR/MOR/RB/707384/2020.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika mahakama ya mwanzo ya CHAMWINO MJINI**

Usimamizi wa mirathi **102/ 2020**
Ombi la **SARAH DANIEL MAPUNDA** kuteuliwa kuwa msimamizi wa mirathi ya marehemu **ERASMUS HERBERT MAPUNDA** Kwa yeyote anayehusika na mirathi hii **TANZANIA BARA**
Watu wote wanaodaiwa kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu huyo wanalikwa kuja na kuudhuria shauri wakitaka mnamo tarehe **01/12/2020** kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hio.

**TAARIFA YA KAWAIDA**
**KATIKA MAHAKAMA YA TANZANIA**
**ILALA/KINYEREZI**
**UTHIBITISHO NA USIMAMIZI WA MIRATHI**
**SHAURI NAMBA LA MWAKA 47/2020**
**MAOMBI NA BARUA ZA USIMAMIAJI WA MIRATHI YA HENDRICK SUDI MFUNDIRI**
**MAREHEMU WA....GEOFREY HENDRICK MFUNDIRI MUOMBAJI**

**TAARIFA YA KAWAIDA**
**(KANUNI YA 75)**

Watu wote wanaodai kuwa na haki katika mirathi ya marehemu aliyetajwa hapo juu wanakaribishwa kufika na kuangalia mashauri haya katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa barua za usimamizi kwa mwombaji aliyetajwa hapo juu
Mapingamizi yoyote kuhusu maombi haya yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya tarehe **01/12/2020**
Wosia wa marehemu huyo aliyetajwa umewekwa amana na uwazi kuwa upo mahakamani.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA MWANZO KAWE**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

Katika mahakama ya mwanzo **KAWE**
Usimamizi wa mirathi 263 2020
Ombi la **LILIAN IDD MSHANA** na **FATUMA IDD MSHANA**
Msimamizi wa mirathi ya marehemu **DIHINA IDD MSHANA**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe 18/11/2020 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo **DIHINA IDD MSHANA**
Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**DEOGRATIUS BABU MCHOMVU**
anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **TOYOTA** yenye namba za usajili **T 834 DNN** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilicho karibu.
Taarifa ya polisi
**DAR/STA/RB/686547/2020**

**PUBLICATION SUMMONS**
**IN THE DISTRICT COURT OF BUKOBA**
**AT BUKOBA**
**MISC.CRIMINAL APPLICATION NO 25 OF 2020**
*(Arising from criminal case No 7 of 2020 at Rubale primary court)*

**PRUDENCE BENEDICTO........................APPLICANT**
**Versus**
**YASIN SWAIBU..................................RESPODENT**
**ONESMO GARASIAN........................RESPODENT**
**STEPHANO SIMON.........................RESPODENT**

**NOTICE TO APPEAR AND HEARING**

**TO:YASSIN SWAIBU OF KYAITOKE-0715007268**

**TAKE NOTICE** that the mentioned case has been set down for mention on the 13 day of November,2020 at 8:30 o'clock in the forenoon,Before **Hon.F.A. KAIJAGE-RM** your presence is therefore required on the date and the time indicated.
Given under my hand and the seal of the court this 27th day of Septemba,2020.

RESIDENT MAGISTRATE
BUKOBA

115993702

**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**KANDA YA MWANZA**
**SHAURI LA MADAI YA RUFAA YA NDOA NO. 12 YA MWAKA 2019**

**FATUMA WAZIRI..........................MLETA RUFAA**
**DHIDI YA**
**KIYA MBAYO..................MJIBU RUFAA**

**Kwa:**

**KIYA MBAYO**

**KUITWA SHAURINI**
Unaarifiwa kuhudhuria hapa Mahakamani tarehe 17/11/2020 kuja kusikiliza shauri la rufaa lililofunguliwa na mleta rufaa dhidi yako.
Unatahadharishwa kuwa endapo hautofika siku hiyo shauri litasikilizwa upande mmoja dhidi yako na kutolewa maamuzi.
Hati hii imetoleta kwa mkono wangu na chapa ya mahakama leo tarehe 30/9/2020.
**NAIBU MSAJILI**
**MAHAKAMA KUU TANZANIA**
**MWANZA**

## TANGAZO
## KUPOTEA OFA YA KIWANJA

**Lazaro Maingu Njarabi,** anatangaza kupotelewa na Ofa ya kiwanja Namba **107 ,Kitalu "U"** Kambarage manispaa ya Shinyanga.
Kwa yeyote atakae iona atoe taarifa kituo cha Polisi kilichopo karibu, au awasiliane na Lazaro Maingu Njarabi kwa simu namba **0713501055**.

**RB Namba:RB/SHY/2020, Control Namba 9910819632819.**

## TANGAZO
## KUPOTEA OFA YA KIWANJA

**Kitija Kulamiwa Sendama,** anatangaza kupotelewa na Ofa ya kiwanja namba **309 Kitalu "GG"** Kitangili Manispaa ya Shinyanga.
Kwa yeyote atakae iona atoe taarifa kituo cha Polisi kilichopo karibu, au awasiliane na Kitija Kulamiwa Sendama kwa simu namba **0622515459**.

**RB Namba: RB/SHY, 2020, Control namba 9910819617361.**

**Kwa Habari Motomoto**
usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku
Tupigie
0782253676
Nipashe
MWANGA WA JAMII

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji
THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KIMATAIFA

## Mapigano yashika kasi Ethiopia wananchi wahaha

**ADDISABABA,** Ethiopia

MAPIGANO makali yanaendelea Tigray, Ethiopia, wakimbizi wakikimbilia Sudan, huku Umoja wa Afrika (AU) ukiendelea kutoa wito wa kusitishwa mapigano hayo.

Jeshi la Ethiopia linaendelea kushambulia makundi ya wapiganaji katika eneo hilo, baada ya viongozi wa Tigray kukaidi mamlaka ya Waziri Mkuu, Abiy Ahmed.

Takribani watu 2,500 wamekimbilia Sudan kutoka Ethiopia kufuatia mapigano hayo katika eneo la Tigray, huku maofisa wakielezea wasiwasi wao kwamba huenda idadi ya watu wanaokimbia mapigano hayo ikaongezeka kwa kasi.

Mamia ya watu wamekufa kutokana na mashambulizi ya angani, huku hali ya wasiwasi ikiongezeka kwamba huenda Ethiopia ikarudi tena katika vita vya wenyewe kwa wenyewe kutokana na uhasama mkubwa uliopo kwa sasa kati ya jamii ya Tigray na Oromo.

Shirika la habari la serikali limeripoti kwamba, wanajeshi wa serikali wamedhibiti Uwanja wa Ndege wa Humera, karibu na mpaka na Sudan na Eritrea.

Shirika la habari la FANA, linaloshirikiana na serikali, limeripoti kwamba wanajeshi 17 wamekamatwa kwa kutatiza mfumo wa mawasiliano unaotumika na wanajeshi wa serikali ya Jimbo la Tigray na kuhatarisha usalama wa jeshi la jimbo hilo TPLF.

Abiy, ambaye alishinda tuzo la amani la Nobel mwaka 2019, aliamurisha mashambulizi ya angani na kutuma wanajeshi Tigray wiki iliyopita, akishutumu Jeshi la TPLF kwa kushambulia kambi ya jeshi.

Utawala wa Tigray unadai kwamba serikali ya Abiy inawakandamiza na ilichukua hatua za kidikteta kuahirisha uchaguzi mkuu. **VOA**

# Burundi yapiga mnada mali za wapinzani

**BUJUMBURA,** Burundi

**Familia nyingi zitapokonywa kila kitu, na watoto ambao nyumba za familia zao zitauzwa, watajikuta wakiranda mitaani.**

WIZARA ya Sheria ya Burundi imetoa tangazo kupitia redio na televisheni ya taifa, ikiwaalika wanunuzi katika mnada wa mali za wapinzani zinazoshikiliwa na mahakama.

Mali zinazouzwa ni za wapinzani wa serikali wapatao 30, ambazo zilikamatwa Mei, mwaka jana chini ya amri ya mahakama.

Wapinzani hao walipinga hatua ya Rais wa zamani wa Burundi, hayati Pierre Nkurunziza kuwania muhula wa tatu mwaka 2015.

Miongoni mwao ni aliyekuwa Makamu wa Rais Bernard Busokoza, aliyekuwa msemaji wa chama tawala cha CNDD-FDD, Onesme Nduwimana, mpinzani maarufu Alexis Sinduhije, na Mkurugenzi wa Kituo cha kuwalea watoto yatima cha Maison Shalom, Marguerite Barankitse.

Wengine kwenye orodha ya watu ambao mali zao zinauzwa katika mnada huo ni wanajeshi tisa, waliohukumiwa kifungo cha maisha kwa hatia ya kuhusika katika jaribio la mapinduzi lililoshindwa Mei 13, 2015.

Wanajeshi hao ni Jenerali Godefroid Niyombare na Jenerali Cyrille Ndayirukiye, Waziri wa zamani wa ulinzi, aliyekuwa miongoni mwa viongozi wa mapinduzi hayo.

Kulingana na taarifa iliyotolewa na Mwenyekiti wa Shirika la kutetea uhuru wa asasi za kiraia nchini Burundi, Vital Nshimirimana, mnada huu utaacha athari zisizoweza kutathminika.

Alisema familia nyingi zitapokonywa kila kitu, na watoto ambao nyumba za familia zao zitauzwa, watajikuta wakiranda mitaani.

Chanzo kimoja ambacho hakikutaka kutajwa jina, kimeiambia DW kuwa waandishi wa habari ndani ya Burundi hawaruhusiwi kuripoti mchakato wa mnada huo. **DW**



Rais wa Burundi, Evariste Ndayishimiye. **PICHA: AFP**

# Biden aendelea na mpango wa kuunda serikali

**WASHINGTON,** Marekani

RAIS mteule wa Marekani, Joe Biden, anaendelea na mchakato wa kuujenga utawala wake, huku rais aliyeshindwa katika uchaguzi uliopita, Donald Trump akiendelea kuwasilisha kesi mahakamani.

Jana, Joe Biden (pichani) alipanga kukutana na kikundi cha washauri wake, ambao wanamsaidia kuweka msingi wa utawala mpya, na kumuandaa kula kiapo cha kuchukua madaraka ifikapo Januari 20 mwakani.

Miongoni mwa washauri hao ni wataalamu wa masuala ya kibenki na kifedha, wanaotoka chama chake cha Democratic pamoja na wale wenye mrengo usio wa kihafidhina.

Rais huyo mteule pia anawatumia watu waliopangilia sheria kali za kimazingira wakati wa utawala wa Rais Barack Obama.

Wakati huo huo, Biden amesema hatua ya Rais Donald Trump kukataa kushindwa katika uchaguzi mkuu wa urais, ni aibu.

Lakini, Biden ambaye amekuwa akiwasiliana na viongozi wa kimataifa amesisitiza kwamba hakuna kitu kitakachozuia uhamisho wa madaraka.

Rais mteule aliulizwa na waandishi wa habari siku ya Jumanne kile anachofikiria kuhusu hatua ya Rais Trump kukubali kwamba alishindwa katika uchaguzi.

"Nadhani ni aibu, kusema kweli, kile ninachoweza kusema, kwa heshima, Nadhani hatua hiyo haitasaidia kudumisha hadhi ya rais atakapoondoka madarakani. Mwisho wa siku, mbivu na mbichi itajulikana Januari 20," alisema Biden, akiashiria siku ya kuapishwa.

Biden amekuwa akiwasiliana kwa njia ya simu na viongozi wa kigeni anapojiandaa kuingia rasmi ofisini. Waziri Mkuu wa Uingereza, Boris Johnson, Kiongozi wa Ireland, Taoiseach Micheál Martin, Rais wa Ufaransa Emmanuel Macron na Kansela wa Ujerumani, Angela Merkel ni miongoni wa viongozi aliofanya nao mazungumzo.



Kwenye mazungumzo hayo, Biden alisema: "Nawafahamisha kwamba Marekani imerejea tena ulingoni. Tunarudi tena katika nafasi yetu mchezoni."

Biden na Makamu wa Rais wake mteule, Kamala Harris wanaendelea na maandalizi ya kuingia madarakani.

Lakini shirika dogo linaloongozwa na washirika wa Rais Trump linadaiwa kulimaza mpango huo.

Shirika hilo linalosimamia huduma zote za serikali kuu ikiwa ni pamoja kufadhili na kusaidia utawala mpya unaoingia madarakani kufikia idara za serikali, mpaka sasa limekataa kumtambua rasmi Biden kama rais mteule.

Hata hivyo, Biden amesema: "Hatuoni kitu chochote kikirudisha nyuma mipango yetu, kusema kweli."

Mwanzoni mwa wiki, Trump aliweka ujumbe mara kadhaa katika mtandao wa kijamii wa Twitter kwa kutumia herufi kubwa akielezea namna shughuli ya kuhesabu kura ilivyokumbwa na udanganyifu, kusema kwa majigambo: "Tutashinda!"

Rais Trump amekuwa akitoa madai ambayo hayajathibitishwa akisema Biden anaweza tu kushinda uchaguzi ambao umechakachuliwa kwa njia ya ufisadi, lakini hakuna ushahidi wowote uliotolewa kuthibitisha madai hayo. **BBC**

HABARI MICHEZO

# DEPAY AZUIWA BARCA JANUARI



**LYON,** Ufaransa

MEMPHIS Depay hataondoka Lyon katika dirisha la usajili la Januari licha ya kuhusishwa na kuwaniwa na Barcelona, kwa mujibu wa Jean-Michel Aulas.

Barca walikuwa wakihusishwa sana na usajili wa Depay baada ya kocha wa zamani wa timu ya Taifa ya Uholanzi, Ronald Koeman kuchukua mikoba Agosti, mwaka huu, lakini nyota huyo wa zamani wa Manchester United alibaki kwa miamba hao wa Ligue 1.

Miamba ya kule Catalunya inaangalia uwezekano wa kumsajili mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26, baada ya Ansu Fati kuumia goti na anatarajiwa kuwa nje ya dimba kwa miezi minne.

Mkataba wa Depay na Lyon unatarajiwa kumalizika Juni na Rais wa Klabu hiyo, Aulas amesisitiza hawatamruhusu kuondoka mapema.

"Memphis ni mcheza wa aina yake. Yeye ndiye anayeisukuma klabu, pamoja na wachezaji wengine," alisema Aulas akiiambia RMC.

"Nilikuwa wa kwanza kusema hatakwenda Barcelona, hakuna mtu aliyenisikiliza mimi wakati wa dirisha la usajili kwa sababu kila mtu alifikiri ataweza kuondoka."

Depay ameendelea kuwa kwenye kiwango cha kuvutia kwa miamba hiyo ya Ligue 1 licha ya uhamisho wake kushindika kwenda kule Barca.

# Maradona kuruhusiwa kutoka hospitali

**BUENOS AIRES,** Argentina

DIEGO Maradona anatarajiwa kuruhusiwa kutoka hospitali alikolazwa wakati wowote, kwa mujibu wa daktari wake binafsi, Leopoldo Luque.

Afya ya Maradona imeendelea kuimarika baada ya kufanyiwa upasuaji wa kichwa wiki iliyopita, siku moja baada ya kukimbizwa hospitali.

Luque ametoa taarifa zaidi juu ya maendeleo ya gwiji huyo wa Argentina na Napoli mwenye umri wa miaka 60, ambaye ni kocha wa Klabu ya Gimnasia y Esgrima La Plata.

"Diego anaendelea vizuri sana, operesheni aliyofanyiwa imekuwa na mafanikio makubwa," alisema Luque akiwaambia waandishi wa habari.

"Kwa sasa inafikiriwa kumruhusu kutoka hospitali, na yeye kwa uhakika kabisa anataka kuondoka na tayari ameonyesha nia hiyo.

"Hali ya mgonjwa inaimarika na anapoomba kuruhusiwa kutoka hospitali, madaktari wanakuwa hawana pingamizi kama wamejiridhisha.

"Shukrani kubwa kwa timu ya madaktari, lakini juu ya yote ni sapoti ya mazingira, familia na ndugu.

"Kuruhusiwa kwa Diego ni suala la muda tu, hataruhusiwa leo, lakini mapema hivi karibuni."

Maradona, ambaye alishinda Kombe la Dunia na Argentina mwaka 1986 na kuiongoza Napoli kushinda mataji mawili ya Serie A, amekuwa kocha wa klabu ya Ligi Kuu ya Argentina, Gimnasia tangu mwaka 2019.





# Barthez aibukia Toulouse

**TOULOUSE,** Ufaransa

GOLIKIPA wa zamani wa Ufaransa, Fabien Barthez, amerudi katika klabu yake ya zamani ya Toulouse kwa kipindi chote cha msimu kilichobaki kama mshauri.

Barthez atafanya kazi ya kocha wa magolikipa wa Toulouse, Patrice Garande na ofisa wa akademi, Denis Zanko kwa klabu hiyo iliyopo Ligi Daraja la Kwanza, Ligue 2, ambako ndipo aliponza kucheza soka la kulipwa mwaka 1991.

Baada ya kuondoka Toulouse alipokaa kwa mwaka mmoja, Barthez alikwenda kushinda taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya na Marseille, na taji la Ligi Kuu ya England na Manchester United baada ya kushinda Kombe la Dunia mwaka 1998 na Euro 2000 akiwa na kikosi cha Ufaransa.

"Hisia zangu halisi zimenihamasisha kufanya kazi ya ushauri. Natarajia kutumia uzoefu wangu kuweka hapa kwa kushirikiana na benchi la ufundi, na kocha wa makipa wa kikosi cha kwanza na akademi," alisema Barthez katika taarifa yake.

"Ningependa kumshukuru Rais (Damien) Comolli, uongozi wa timu pamoja na Patrice Garande, Rudy Riou na Denis Zanko kwa kuniamini na kunikaribisha."

Toulouse walishuka daraja kutoka Ligue 1 hadi Ligue 2 msimu uliopita.

HABARI MICHEZO

# Deschamps atoa sababu kumuita mtoto wa Thuram

**PARIS,** Ufarans

DIDIER Deschamps amesema Marcus Thuram, anastahili kuwapo kwenye kikosi cha Ufaransa na ameitwa kwa faida na si sababu ya baba yake.

Thuram, ni mtoto wa Lilian Thuram, alikuwa sehemu ya kikosi cha Ufaransa kilichocheza mechi ya kirafikiri na Finland jana Jumatano.

Straika huyo wa Klabu ya Borussia Monchengladbach ya Ligi Kuu ya Ujerumani, ameanza vizuri msimu huu, akifunga mabao matatu na kutoa pasi za mwisho mbili katika mechi 11, yakiwamo mawili dhidi ya Real Madrid.

Amehusika katika mabao 20 kwenye Bundesliga tangu alipojiunga pale Gladbach msimu uliopita.

Deschamps alizungumzia kuhusu kipaji cha Thuram wakati akitangaza kikosi cha Ufaransa wiki iliyopita na alisisitiza mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23 anang'ara kwa juhudi zake na si kwa kivuli cha baba yake, ambaye aliichezea Ufaransa mechi 142.

"Ni kama baba yake, nampenda, lakini tunazungumza kuhusu Marcus. Anatengeneza jina lake mwenyewe," amesema Deschamps akiwaambia waandishi wa habari jana kabla ya kuivaa Finland.

"Anakwenda vizuri sana, hivyo kuwapo kwake kwenye kikosi cha Ufaransa si kwa sababu ya baba yake."



# THIAGO AZICHAMBUA EPL, SERIE A, LIGUE 1



**LONDON,** England

THIAGO Silva amesema mechi zake za mwanzo kwenye Ligi Kuu ya England zilimuumiza kichwa, lakini anatarajia atazongezewa mkataba pale Chelsea.

Silva alijiunga na Chelsea kwa uhamisho huru Agosti, mwaka huu baada ya mkataba wake kumalizika kule Paris Saint-Germain.

Nahodha huyo wa zamani wa PSG ana umri wa miaka 36, na tayari amekuwa na mchango pale Stamford Bridge, akiiwezesha kutofungwa katika mechi zake nane za kwanza kwenye mashindano yote na kuwasaidia Blues hao kujivuta hadi nafasi ya tano kwenye msimamo wa ligi.

Akiwa na kikosi cha Brazil kwenye mechi za kimataifa, Silva aliulizwa namna gani anaweza kulinganisha soka la Uingereza na Ligue 1 na lile la Serie A, ambako aliichezea AC Milan.

"Ni ligi tatu zenye aina tofauti kabisa ya soka," alisema akiwaambia waandishi wa habari.

"Nilipata uzoefu mkubwa sana wa kujifunza kule Italia, moja ya shule bora kabisa kwenye suala la ulinzi.

"Pia nilikuwa na uhusiano mzuri na (Paolo) Maldini na (Alessandro) Nesta, ambapo nilicheza nao kwa miaka miwili, hivyo nilikuwa na wakati wa kujifunza mechi kutoka kwao.

"Soka la Ufaransa, halitumii nguvu kubwa na PSG ni kama imetawala soka lote la pale.

"Na sasa nipo kwenye soka la Uingereza, mechi mbili zilizopita ziliniumiza sana kichwa kwa sababu ni ligi inayotumia nguvu na kasi kubwa sana, iko tofauti sana na ligi hizi mbili.

"Nimejifunza kwamba ninachotakiwa kufanya ni kujituma sana kwenye mazoezi."

# *Shaw benchi mwezi mmoja*

**MANCHESTER,** England

MANCHESTER United imethibitisha kwamba, mlinzi wake wa kushoto, Luke Shaw, anakabiliwa na uwezekano wa kuwa nje ya dimba kwa mwezi mmoja baada ya kuumia nyama za paja wakati wa mchezo dhidi ya Everton.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25, alitolewa dakika ya 67 wakati United wakishinda mabao 3-1 pale Goodison Park katika mchezo ambao alimtengenezea bao Bruno Fernandes ambaye alifunga la pili.

Hiyo ilikuwa ni mechi ya pili mfululizo kwa mchezaji huyo wa kimataifa wa England aliyeichezea mechi nane kutoa pasi ya mwisho ya bao, akiwa ameshindwa kufanya hivyo katika mechi nane zilizopita katika mashindano yote msimu huu.

Shaw anatarajiwa kukosa mchezo wa Ligi Kuu dhidi ya West Brom, Southampton na West Ham, pamoja na ule wa Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Istanbul Basaksehir, Paris Saint-Germain na RB Leipzig.

Hata hivyo, Ole Gunnar Solskjaer ataweza kumtumia Alex Telles, ambaye amecheza mechi moja tu tangu ajiunge na timu hiyo akitokea Porto Oktoba mwaka huu.

"Tunatarajia kumkosa Shaw kwa mechi zetu zijazo, kwa sababu aliumia kwenye mchezo dhidi ya Everton," alisema Solskjaer akiwaambia waandishi wa habari.



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# LEONARDO AMVUTA RONALDO KWA PSG

## Tunatakiwa kujiandaa, tuna orodha yetu, lakini yasiyotarajiwa yanaweza kutokea...

**PARIS,** Ufaransa

PARIS Saint-Germain inaweza kumnunua, Cristiano Ronaldo na wawe tayari kwa "yasiyotarajiwa", amesema Mkurugenzi wa Soka wa klabu hiyo, Leonardo.

**Ronaldo ameshinda mataji ya Ligi Kuu England, LaLiga na Serie A akiwa na Manchester United, Real Madrid na Juventus kwa nyakati tofauti.**

Lakini mshindi huyo mara tano wa Ballon d'Or anatajwa kama anaangalia uwezekano wa kutafuta timu nyingine baada ya kujiunga na Juve miaka miwili iliyopita, huku PSG ikitarajiwa kuwa moja ya klabu zinazomwania.

Miamba hao wa Ligi Kuu ya Ufaransa, Ligue 1, tayari wameshinda kwa kuwasajili wachezaji wawili ghali zaidi duniani, Neymar na Kylian Mbappe.

"Katika soka la leo, hatuwezi kujua," alisema Leonardo wakati wa mahojiano ya maswali na majibu katika mitandao ya kijamii ya PSG.

"Kama kesho Cristiano Ronaldo akiamka na kusema, 'nataka kwenda kucheza sehemu nyingine', nani anaweza kumnunua? Ni mzunguko uliofungwa. PSG imeingia kwenye mzunguko huo.

"Kama kawaida, kuna nafasi, na hali halisi. Tunatakiwa kujiandaa kwenye dirisha la usajili na hivyo ndivyo tunavyofanya.

"Tuna vipaumbele vyetu, orodha yetu, lakini yasiyotarajiwa yanaweza kutokea."

Juve wanamatumaini Ronaldo hataondoka hivi karibuni kwani anabaki kuwa mchezaji nguzo kwao katika umri wake wa miaka 35.

Mshambuliaji huyo wa Ureno alikosa mechi mbili za Ligi Kuu ya Italia, Serie A, baada ya kukumbwa na virusi vya corona na zote mbili 'Bianconeri' hao walitoka sare.

## ZISIKUPITE

### NEYMAR KUFUNGWA UPYA

KLABU ya PSG imeanza mazungumzo ya kumpa mkataba mpya mshambuliaji wa Brazil, Neymar, huku mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28, akiripotiwa kufurahia jambo hilo. ***(ESPN)***

### ARSENAL YAMWANIA BRENNER

ARSENAL ni miongoni mwa baadhi ya klabu ambazo zinamwania mshambuliaji wa Sao Paulo na Brazil, Brenner, mwenye umri wa miaka 20. ***(Calciomercat)***

### CARAGHER: POGBA AUZWE

ALIYEKUWA mlinzi wa Liverpool, Jamie Caragher anaamini kwamba Manchester United inapaswa kumuuza kiungo wa kati wa Ufaransa, Paul Pogba 27. ***(Talksport)***

### EVANS KUONGEZEWA MKATABA

LEICESTER City imefungua mazungumzo kuhusu mkataba mpya na mlinzi, Jonny Evans. Raia huyo wa Ireland Kaskazini mwenye umri wa miaka 32, anaingia katika mwaka wa mwisho wa mkataba wake wa miaka mitatu. ***(Athletic)***

### PEPE AILALAMIKIA ARSENAL

WINGA wa Ivory Coast, Nicolas Pepe, mwenye umri wa miaka 25, amelalamika kuhusu muda mchache anaopewa kushiriki katika mechi kwenye klabu ya Arsenal. ***(Canal Plus, via Mirror)***

### DE BOER AMFUNGUKIA DE BEEK

KIUNGO wa kati wa Uholanzi, Donny van de Beek, mwenye umri wa miaka 23, anataka kuichezea zaidi Manchester United, lakini huenda akawa na wakati mgumu kuingia katika kikosi cha kwanza cha timu hiyo, kwa mujibu wa kocha Frank de Boer. ***(Sun)***

### UNITED WAMRUDIA GREALISH

KLABU ya Manchester United huenda ikawasilisha ombi la kumsajili kiungo wa kati wa Aston Villa na England, Jack Grealish mwenye umri wa miaka 25, iwapo Pogba ataondoka pale Old Trafford. ***(Manchester Evening News)***

### BELLINGHAM ATAJWA ARSENAL

ARSENAL ilikaribia kumsajili kiungo wa kati wa Borussia Dortmund, Jude Bellingham mwenye umri wa miaka 17, kutoka klabu ya Birmingham City mwaka 2019. ***(Sky Sports, via Independent)***

### KELLEHER KUONDOKA LIVER

GOLIKIPA wa Liverpool na Ireland Kaskazini, Caoimhin Kelleher, mwenye umri wa miaka 21, anataka kuondoka katika klabu hiyo kwa mkopo wakati wa dirisha la usajili la Januari. ***(Liverpool Echo)***

### WILSHERE KUTOJIUNGA SPURS

KIUNGO wa zamani wa Arsenal, Jack Wilshere, mwenye umri wa miaka 28, amesema hatoweza kujiunga na Tottenham Hotspur kutokana na uhusiano wake na 'Washikabunduki' wa London. ***(Goal)***

### YAMWANIA SZOBOSZLAI

KLABU ya Arsenal imeanzisha mazungumzo na kiungo wa kati wa Red Bull Salzburg, Dominik Szoboszlai mwenye umri wa miaka 20. ***(Football London)***

## HABARI MICHEZO

# MAGARE YADHAMINI ROCK CITY MARATHON

**Na Mwandishi Wetu,** MWANZA

KAMPUNI ya Magare inayohusika na uhandisi wa umeme, mitambo viwandani na migodini jijini Mwanza imekabidhi hundi yenye thamani Sh. milioni 15 kwa waandaaji wa Rock City Marathon ikiwa ni udhamini wao katika kufanikisha mbio hizo zinazotarajiwa kufanyika Novemba 29, mwaka huu, eneo la Rock City Mall jijini hapa.

Akikabidhi hundi hiyo jana kwa waandaaji wa mbio hizo, Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Magare, Mabula Magangila, alisema udhamini huo unalenga kuunga mkono jitihada za wadau wengine pamoja na serikali kwa ujumla katika kuhamasisha michezo na utalii wa ndani hapa nchini.

"Kimsingi tumevutiwa na agenda ya mbio hizi ya kutangaza utalii wa ndani na kukuza sekta ya michezo nchini. Utalii ni moja ya nguzo muhimu katika ukuaji wa uchumi wetu. Pamoja na kuwa sehemu ya wadhamini wa mbio hizi pia tutashiriki kikamilifu ambapo jumla ya wafanyakazi 300 tukiwamo viongozi waandamizi na washirika wetu kibiashara tutashiriki kwenye mbio hizi," alisema.

**Alisema ili kutangaza utalii wa ndani kampuni yake itaendelea kushirikiana na waandaaji wa mbio hizo kuhakikisha zinafanikiwa kuvutia zaidi washiriki kutoka ndani na nje ya nchi ambao ujio wao jijini humo hautaishia katika kuimarisha sekta ya utalii pekee bali pia utafungua milango ya mahusiano ya kibiashara.**

Akizungumza baada ya kupokea hundi hiyo, Mratibu wa Mbio za Rock City Marathon Kanda ya Ziwa, Magdalena Laizer, pamoja na kuishukuru Kampuni ya Magare kwa kuunga mkono mafanikio ya mbio hizo, alisema ushiriki wao wanaofanya kazi na wadau mbalimbali zikiwamo kampuni za kimataifa, utasaidia kuzitangaza mbio hizo nje ya nchi.

"Ushiriki wa kampuni hii ya Magare iliyojijengea heshima kubwa kwenye sekta ya ujenzi hususan uhandisi wa umeme na mitambo viwandani na migodini, utatusaidia pia kuvutia wadau na washiriki kutoka nje ya nchi, hatua ambayo ni muhimu katika kufanikisha agenda yetu ya kutangaza utalii wa ndani hususan Kanda ya Ziwa," alisema.

Alisema maandalizi ya mbio hizo tayari yamekamilika huku ushiriki wa viongozi mbalimbali wa serikali wakiwamo wabunge wateule, wakuu wa mikoa ya Kanda ya Ziwa ukiwa ni miongoni mwa vivutio vikubwa vinavyotarajiwa kupamba mbio hizo.

"Tunatarajia kwamba viongozi hawa wa kiserikali pamoja na wadhamini na wadau wetu wengine wakiwamo Kampuni za TIPER, Pepsi, Bodi ya Utalii Tanzania (TTB), Under The Same Sun (UTSS), Hospitali ya Bugando, CF Hospital, Hoteli ya Pigeon, Garda World, The Cask na Chuo Kikuu cha Mtakatifu Augustino (SAUT) cha Mwanza watashiriki kikamilifu kwenye mbio hizi.

"Tunatarajia kuwa na washiriki zaidi ya 3,000 wakiwamo wakimbiaji wa kimataifa, wakimbiaji kutoka mashirika mbalimbali, wanafunzi sambamba na wenzetu wenye ualbino watakaoshiriki mbio za Km. 5," aliainisha.

Alisema usajili wa mbio hizo unaendelea kwa njia ya mtandao kupitia tovuti ya mbio hizo pamoja na usajili wa kawaida kupitia vituo mbalimbali vilivyopo mikoa ya Dar es Salaam, Mwanza, Geita, Simiyu, Shinyanga, Dodoma, Arusha huku mikoa zaidi ikiendelea kuongezwa.

"Pamoja na medali, washindi wa kwanza wa mbio za kilomita 21 kwa wanaume na wanawake watajinyakulia Sh. milioni mbili kila mmoja, Sh. milioni 1.3 kwa washindi wa pili na Sh. 700,000 kwa washindi wa tatu, huku washindi wanne hadi kumi nao pia wakiibuka na zawadi za medali na pesa taslimu."

"Kilomita 10 hatutakuwa na zawadi za fedha taslimu isipokuwa washiriki watajipatia medali na fulana. Kuhusu mbio za kilomita tano ambazo zitahusisha washiriki kutoka mashirika na taasisi mbalimbali (corporates) sambamba na washiriki wenye ualbino zawadi za fedha taslimu zitatolewa kwa washindi watatu wenye ualbino pekee," alisema.

## Ntibazonkiza kuanza kazi Yanga Jumanne

**Na Adam Fungamwango**

MCHEZAJI mpya wa Yanga raia wa Burundi, Said Ntibazonkiza, anatarajia kuanza kuitumikia rasmi klabu yake mpya ya Yanga Jumanne ijayo.

Akizungumza jijini Dar es Salaam, Mkurugenzi wa Uwekezaji wa GSM wanaoidhamini Yanga, Injinia Hersi Said, alisema mkataba rasmi wa mchezaji huyo unaanza Novemba 17, mwaka huu pindi mechi za kimataifa zitakapomalizika na baada ya hapo atakuja kujiunga na klabu yake mpya, Yanga.


"Mkataba wake utaanza Novemba 17 baada ya kumalizika kwa mechi za kimataifa, baada ya hapo atakuja kujiunga na timu kwa ajili ya mazoezi, lakini kucheza mechi inategemea na kufunguliwa kwa dirisha dogo la usajili. Hatujapata taarifa linafunguliwa lini, lakini litakapofunguliwa tutafuata taratibu rasmi za yeye kuanza kucheza," alisema Hersi.

Mchezaji huyo alisajiliwa baada ya kumalizika kwa mechi kati ya timu ya Taifa ya Tanzania, Taifa Stars dhidi ya Burundi kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam na Stars kukubali kipigo cha bao 1-0, Oktoba 11, mwaka huu.

Ntibazonkiza anayecheza nafasi ya kiungo mshambuliaji, ndiye aliyefunga bao pekee kwenye mechi hiyo na kuwavutia viongozi wa Yanga ambao walikaa naye mezani na kumalizana.

Katika hatua nyingine, Hersi aliwatoa shaka wanachama na mashabiki wa Yanga kuhusu mchezaji Carlos Carlinhos ambaye alikuwa majeruhi kuwa amepona na ataanza kuonekana rasmi uwanjani Novemba 22, mwaka huu.

"Ameshaanza mazoezi kabla ya mechi dhidi ya Simba, nadhani kocha tu hakuweza kumtumia, lakini sasa ni mzima, panapo majaliwa tumtegemee kucheza Novemba 22, atakuwapo uwanjani kama kocha ataona anafaa kumtumia kwa siku hiyo," alisema mkurugenzi huyo.




Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Magare, Mabula Magangila (kulia), akikabidhi mfano wa hundi yenye thamani ya Sh. milioni 15 kwa Magdalena Laizer ambaye ni Mratibu wa Mbio za Rock City Marathon Kanda ya Ziwa, ikiwa ni udhamini wa kampuni hiyo katika kufanikisha mbio hizo zinazotarajiwa kufanyika Novemba 29, mwaka huu, eneo la Rock City Mall jijini Mwanza. Wanaoshuhudia ni maofisa waandamizi wa kampuni hiyo. **MPIGAPICHA WETU**




Mshindi wa bonasi ya Jackpot, Juma Kidori, kutoka Kondoa, Dodoma akionyesha mfano wa hundi ya Sh. milioni 7.5, baada ya kubashiri kwa usahihi mechi 11 kati ya 13 kwenye Jackpot ya wiki iliyopita. Washindi wa mechi 10 wamezawadiwa Sh. 861,913 na dau la Jackpot ya wiki hii limefika Sh. 284,210,840. **PICHA: SPORTPESA**

## *Hard Rock yatamba kuifumua Chuoni FC*

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

MENEJA wa timu ya Hard Rock, Steven Kapusi, amesema anaratajia kupata matokeo mazuri katika mchezo wao wa kwanza wa Ligi Kuu Zanzibar msimu huu watakapoikaribisha Chuoni Jumapili katika Uwanja wa Gombani Kisiwani Pemba.

Akizungumza na Nipashe jana, Kapusi alisema wamejipanga kuhakikisha mchezo huo wanatoka na alama tatu muhimu katika uwanja huo wa nyumbani.

Alisema kuelekea maandalizi ya Ligi Kuu Zanzibar, timu hiyo imeshacheza michezo sita ya kirafiki na timu za madaraja mbalimbali kwa lengo la kutafuta muunganiko mzuri kati ya wachezaji wapya na wale wa zamani.

"Tumefanya usajili kwa ajili kucheza Ligi Kuu Zanzibar, kama tunavyojua ligi hii ni ngumu na yenye ushindani kulingana na mazingira yetu, tutapambana ili kuhakikisha timu haipotezi katika mzunguko huu wa kwanza.

Alisema anawaheshimu wapinzani wao, Chuoni kwa kuwa ni wazoefu katika ligi hiyo, lakini katika mchezo wa mpira lolote linaweza kutokea ndani ya dakika 90.

# Michezo

Alhamisi Novemba 12, 2020

Nipashe





Leonardo amvuta Ronaldo kwa PSG UKURASA 22

WANGU HUU...



Mshambuliaji wa timu Taifa ya Vijana, Ngorongoro Heroes, Nassor Sadaaw (juu) akiucheza mpira huku akipata upinzani mkali kutoka kwa beki wa timu ya Taifa ya Vijana ya Sudan, kwenye mechi ya kirafiki ya kujiandaa na michuano ya vijana Afrika Mashariki na Kati itakayofanyika mwezi ujao jijini Arusha, ambayo ilipigwa katika Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Simba ruksa kuongeza nyota wapya 10 - CAF

## ●●● Kanuni mpya zatolewa Ligi ya Mabingwa na AFCON kutokana na janga la corona, sasa...

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI Simba ikiwa ni miongoni mwa klabu zinazojiandaa na michuano ya Ligi ya Mabingwa, Shirikisho la Soka barani Afrika (CAF), limeongeza idadi ya wachezaji wanaoweza kuzitumikia klabu zinazoshiriki michuano yake yote kutoka 30 hadi 40, limeeleza.

**Simba itaifuata Plateau United ya Nigeria kwenye mechi ya awali ya hatua ya mtoano itakayopigwa kati ya Novemba 27-29 kabla ya kurudiana hapa nchini kati ya Desemba 4-6, mwaka huu wakati tarehe hizo Namungo yenyewe ikianzia nyumbani dhidi ya Al Rabita FC ya Sudan kwenye Kombe la Shirikisho Afrika.**

Hatua hiyo imefikiwa kutokana na miongozo ya itifaki za afya za FIFA na CAF dhidi ya COVID-19 na kwa kuelekea kuanza tena kwa mashindano, wachezaji wanaopimwa na kubainika kuwa na virusi vya corona hawaruhusiwi kushiriki kwenye mechi.

Katika muktadha huo, Kamati ya Dharura ya CAF, imeruhusu timu tofauti zinazoshiriki mashindano ya shirikisho hilo kuwa na idadi ya kutosha ya wachezaji wa kucheza mechi, na imepitisha hatua hiyo kutokana na mapendekezo ya Kamati ya Maandalizi ya AFCON iliyofikia uamuzi ufuatao:

Kwa mashindano ambayo kanuni zimeweka orodha na idadi ndogo ya wachezaji (Mfano: michuano ya ndani ya klabu, mashindano ya mfumo wa mtoano ambao huishia kwa mshindi wa fainali kuwa bingwa...), kutakuwa na ongeza la wachezaji 10; (ikiwa kwa mfano kanuni zimeweka idadi ya wachezaji 30 wataongezwa hadi 40.

Kwa mashindano ambayo kanuni zinaruhusu marekebisho ya orodha ya wachezaji kutoka mechi moja kwenda nyingine (mfano: Kufuzu AFCON kwa wanaume na wanawake nk): vyama ama mashirikisho yanaweza kusafiri na idadi ya wachezaji isiyo na kikomo ambayo itawaruhusu kuziba pengo pindi mchezaji yeyote akibainika kuwa na COVID-19.

Kutokana na ongezeko hilo la idadi ya wachezaji kwenye orodha, sheria ifuatayo, ambayo ni kwa mujibu wa sheria za mchezo itatumika kwa mashindano yote ya CAF: Timu italazimika kuhakikisha inawasilisha wachezaji wasiopungua 11 (pamoja na kipa mmoja + na wanne wa 'sab' kufanyia mabadiliko) kushiriki kwenye mechi na hii ni bila kujali idadi ya wachezaji ambao wangepimwa na kubainika kuwa COVID-19.

Iwapo timu haitaweza kushiriki kwenye mechi, matokeo ya mechi yataamuliwa kulingana na vigezo vifuatavyo:

Mosi, ikiwa timu haina idadi ya chini ya wachezaji (wachezaji 11 wakiwamo kipa mmoja na wanne wa 'sab' mabadiliko), timu hiyo itachukuliwa kuwa imepoteza kwa mabao 2-0. Pili, ikiwa timu inayoshiriki haiwezi kusafiri kwenda kwa nchi mwenyeji ama uwanjani kwa sababu ya kusafiri au kizuizi chochote kinachohusiana na COVID-19, timu inayoshiriki itachukuliwa kuwa imepoteza mechi kwa mabao 2-0.

Tatu, Endapo timu mwenyeji haiwezi kuandaa mechi au haiwezi kuidhinishwa na serikali yake kupokea timu nyingine, timu mwenyeji itachukuliwa imepoteza mechi kwa mabao 2-0.

Nne, Kwa kesi za kipekee, kamati ya kuandaa mashindano itashauriwa kuchukua uamuzi wa mwisho. Walakini, ikiwa serikali ya chama cha mwenyeji itaidhinisha kwamba mechi zinaweza kuchezwa na watazamaji, shirikisho mwenyeji lazima lipate idhini ya mapema kutoka CAF. Idadi ya watazamaji haitazidi asilimia 50 ya uwezo wa uwanja.

Kwa mujibu wa CAF, hatua hizo ni bora na zinafaa tu wakati wa mazingira ya sasa ya janga corona linalosababisha ugonjwa wa COVID-19.

# Yanga yafunguka Senzo kushikiliwa

**Na Faustine Feliciane**

ALIYEKUWA Mtendaji Mkuu wa klabu ya Simba ambaye kwa sasa yupo ndani ya kampuni inayoidhamini Klabu ya Yanga (GSM) kama mshauri kuelekea mfumo mpya wa uendeshaji wa klabu hiyo, Senzo Mazingisa, jana alishikiliwa na Jeshi la Polisi kwa muda kabla ya kuachiwa.

Mapema jana taarifa za kukamatwa kwa Senzo zilianza kusambaa mchana kwenye mitandao ya kijamii zikimhusisha na tuhuma za upangaji matokeo kwenye baadhi ya michezo ya Ligi Kuu Tanzania Bara.

Kamanda wa Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Lazaro Mambosasa, alipotafutwa kuthibitisha kushikiliwa kwa Senzo alielekeza kutafutwa Kamanda wa Polisi Wilaya ya Kinondoni.

"Jambo hilo nadhani umtafute Kamanda wa Kinondoni, anaweza kukueleza kama ni kweli au la," alisema Mambosasa.

Hata hivyo, alipotafutwa Kamanda wa Kinondoni majira ya saa 11 jioni simu yake ilikuwa haipatikani na wasaidizi wake walieleza kuwa yupo kwenye kikao.

Alipotafutwa Mkurugenzi wa Uwekezaji GSM, Injinia Hersi Saidi, alisema: "Kaka sidhani kama mimi ninapaswa kuulizwa juu ya jambo hilo, sipo kwenye nafasi ya kuelezea jambo hilo nadhani zipo mamlaka nyingine," alisema.

Hata hivyo Msemaji wa Klabu ya Yanga, Hassan Bumbuli alikiri kuwa Senzo alishikiliwa na Polisi, lakini aliachiwa jana hiyo hiyo baada ya kutoa maelezo yake.

"Ishu ni ile ile aliyokamatwa nayo Hashim Mbaga (aliyekuwa Mkurugenzi wa Wanachama wa Klabu ya Simba), lakini Senzo ametoa maelezo yake na kurejea ofisini kwenye majukumu yake, ni hivyo tu wala sio kweli kuwa anashikiliwa mpaka sasa," alisema Bumbuli.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >